

FAHAMU YAFUATAYO KUHUSU NDOTO UNAZOTA ILI UFANIKIWE KIMAISHA

Na Mwl Mwakasege. Dodoma Uwanja wa Barafu April 2-9 2017.

Notes from Felix Mbwanji and Glory Mlay



FAHAMU YAFUATAYO KUHUSU NDOTO UNAZOOTA ILI UFANIKIWE KIMAISHA

SIKU YA KWANZA

LENGO: KUIMARISHA UHUSIANO WAKO NA MUNGU KATIKA KRISTO YESU ILI UFANIKIWE KIMAISHA

☞ Somo hili litatoa majibu ya Maswali ya watu wengi kadri Mungu atakavyotusaidia.

☞ Hili somo halipatikani kirahisi rahisi na miaka ile tulivyoanza tulipata shida sana. Na hata vitabu havipo vingi sana vinavyoeleza mambo ya ndoto. Kwa hiyo twende pamoja.

Jambo la 1. Shetani anaweza kutumia ndoto kupandikiza vitu kwako ambavyo usipoving'oa vinaweza kwamisha maisha yako

*Ndipo huyo Elifazi, Mtemani, akajibu na kusema, Basi, nililetewa neno kwa siri, Sikio langu likasikia manong'ono yake. Katika mawazo yaliyotoka *katika maono ya usiku*, Hapo usingizi mzito uwaangukiapo wanadamu. Hofu iliniangukia na kutetema, Iliyotetemesha mifupa yangu yote. Ndipo pepo ilipita mbele ya uso wangu; Na nywele za mwili wangu zilisimama. Hiyo pepo ilisimama kimya, nisiweze kutambua sura zake, Mfano ulikuwa mbele ya macho yangu; Kulikuwa kimya, nami nilisikia sauti, ikinena, **AYUBU. 4:1, 12-16***

☞ Maana ya maono ni ndoto na ndio maana maandiko yanasema

*Kwa kuwa Mungu hunena mara moja, Naam, hata mara ya pili, ajapokuwa mtu hajali. **Katika ndoto, katika maono ya usiku, Usingizi mzito uwajiliapo watu, Katika usingizi kitandani; AYU. 33:14-15***

☞ Hapa kuna vitu vinne yaani kuna

- 1 wazo liliingia ndani yake kwa ndoto
- 2 katika masikio iliingia sauti iliyoharibu usikivu wake
- 3 Hofu ilimwingia
- 4 Mifupa yake ikaanza kutetemeka

Na kuonesha kitu kilichokuja kwake na aliona pepo lililoingiza vitu ndani yake. Tangu siku hiyo hivyo vitu vilimsumbua sana kama hakupata msaada wa kuving'oa basi vilivuruga maisha yake.

Angalizo. Usipuuzie ndoto unayo ota maana inaweza tumika

☞ Kukuletea ujumbe wa Mungu

☞ Kukuletea Maonyo

☞ Au shetani anaweza pandikiza vitu.

MFANO WA PILI

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

*Kukizuka katikati yako nabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, Na tuiquate miungu mingine usiyojua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa BWANA, Mungu wenu, yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda BWANA, Mungu wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. Tembeeni kwa kumfuata BWANA, Mungu wenu; mcheni na kushika maagizo yake na kuisikia sauti yake, nanyi mtumikieni na kushikamana naye. **KUMBU KUMBU. 13:1-4***

Ndoto inaweza tumika na shetani

1. kupandikiza unabii wa uongo kwa kutumia ishara.
2. Wanapewa uwezo wa kushawishi watu wasimfuata Mungu katika Kristo Yesu.

Mara nyingi hatakuja na ndoto atakuja na ishara na utampokea kwa sababu ya ishara au muujiza. Na yeye ataleta na ujumbe na itakuwa ngumu sana kwako kukataa kwa sababu umeona ishara au muujiza. Na lengo kubwa ni kuwa uache kumfuata Mungu na kumpenda Mungu kutapoa na utapoteza hofu ya Mungu

☞ Unapoteza kuambatana na Mungu.

☞ Unatopeteza kusikia Mungu anachosema na utanza kupotea na utanza kusikia neno la mtumishi zaidi bila kufuata neno la Mungu. Na wengi wamekwama hapo.

Watumishi wameacha kumtumikia Mungu kwa sababu waliota ndoto na kuna vitu vilikuja na mbwembwe na wakidhani ni Mungu kumbe sio

MFANO WA TATU.

*Nimesikia waliyoyasema manabii wanaotabiri uongo kwa jina langu, wakisema, **Nimeota ndoto; nimeota ndoto.** Je! Mambo hayo yatakuwa katika mioyo ya manabii wanaotabiri uongo hata lini, manabii hao wenye udanganyifu katika mioyo yao wenyewe? Wanaodhania ya kuwa watawasahaulisha watu wangu jina langu kwa ndoto zao, wanazomhadithia kila mtu jirani yake, kama vile baba zao walivyolisahau jina langu, kwa ajili ya Baali. **YEREMIA. 23:25-27***

Hapa unaona ndoto ilipandikiza

1. Unabii wa uongo
2. Udanganyifu moyoni mwake
3. Alipewa nguvu ya kushawishi watu wa Mungu walisahau jina la Mungu, jina linawakilisha heshima, uwepo au mamlaka aliyonayo mwenye jina kwako.

Mtu akikusahaulisha jina la Yesu.

☞ Hujali tena neno la Mungu

☞ Hutaona thamani wa uwepo wa Yesu.

☞ Hutakuwa na heshima kwa Yesu

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Na chanzo cha haya ni ndoto, na anahadhia watu ili kupandikiza kitu ndani ya mioyo ya watu ili wakae mbali na Mungu.

Nabii aliye na ndoto, na aseme ndoto yake; na yeye aliye na neno langu, na aseme neno langu kwa uaminifu. Makapi ni kitu gani kuliko ngano? Asema BWANA. YEREMIA. 23:28

Kisha akawaambia, Sikizeni basi maneno yangu; Akiwapo nabii kati yenu, Mimi, BWANA, nitajifunua kwake katika maono, Nitasema naye katika ndoto. HESABU 12:6

Ndoto ni njia moja wapo Mungu anatumia kuwapa unabii watu. Na shetani nae anaiga na analeta manabii wa uongo, waalimu na mitume wa uongo.

Kuna manabii wa kweli Mungu anasema nao na kuna nabii wa uongo ambao shetani anaweka.

Pia hii itakusaidia kuchukua **tahadhari na kuweza kutofautisha**. Mambo haya yanahitaji ufutailiaji wa Karibu

Na nilipoanza kufundisha hili somo nimepata kuona ndoto nyingi sana na watu wengi sana wanauliza. Na bado naendelea kufuatilia

Mungu alianza kusema na mimi miaka ile ya 80 na ilinisukuma kufuatilia sana ndoto na wakati ule sijaokoka nilienda kwa waganga na walinipa tafsiri lakini sio kwa usahihi. Ndipo baada ya kuokoka Neema ya Mungu ilianza kunifundisha kwa hatua kwa hatua kwa muda mrefu kidogo ndipo sasa nilianza kufundisha..

MFANO WA NNE.

Kuna mtu aliniandikia kuwa kaota ndoto kuna mtu anakata kwa kisu kidole cha gumba cha mguu wa kulia na baada ya kuamka nilianza kusikia maumivu. miezi 3 baadae kidole kikaaza kuweka weusi pale alipokatwa na palikuwa peusi na kuanza kuwasha na hadi aliponisikia nikifundisha ndipo alianza kuchukua hatua

MFANO WA TANO

Naomba niombee niliota nang'atwa na mbwa mkono wa kushoto na sasa naanza kusikia maumivu hadi kwenye bega na nasikia ganzi.

MFANO WA SITA

Niliota nyoka kaingia mguu wangu wa kushoto na mguu wukaanza kupata shida alipata ganzi na akiingia kwenye maombi tumbo linajaa na kufura

MFANO WA SABA

Kuna mtu alianidika kuwa anaota mara kwa mara akiteleza kuangukia kwenye shimo au maji na mguu huo ndio anateleza kwanza .

Baada ya miezi kadhaa ule mguu ambao ndio unatangeliza ulipata shida na ndipo aligundua kuwa unakidonda..

Mwingine aliota kameza buibui na baada ya muda alianza kukohoa na kazunguka kila hospital ili kutafuta dawa kwa sababu kifua kinamsumbua na haponi. Baada ya kusikia somo hili ndipo alianza kuhusianisha na ndoto aliyoota na akatuandikia

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

✍️ ushuhuda wa mama aliyekuwa na binti yake alikuwa anachemea mguu na walikuja kunisalima nilipokuwa nje ya hospitali moja hapa nchini na nilisikia kumuuliza na alinieza na alisema kaota ndoto kuwa alikuwa anacheza mpira na alipopiga mpira kwenye ndoto aliumia na alipoamka akawa anachecheamea. Na hospitali walipopima hawakuona kitu.

Na nilimuomba na baada ya maombi alipona..

KUNA HATUA ZA KIJUMLA ZA NAMNA YA KUFANYA AU KUOMBA

1.Lazima kuomba toba kwa ajili ya mlango uliofunguka na kuruhusu ndoto kuleta mashambulizi.
Kwa hiyo usijihesabie haki ili umeota ndoto na ikaleta madhara ina maana kuna mlango hapo uko wazi

Kazi ya toba ni .

i) Kuondoa uhalali kwa kiroho wa shetani kukutesa.

ii) Mungu kukusaidia/kupata uhalali wa kukusaidia.

Shetani ili kukushambulia huwa anashambulia kihalali/ kwa hiyo na wewe ili kupambana nae inabidi umuondolee uhalali.

2.Nyunyiza damu ya Yesu kwenye eneo uliloshambuliwa..

Mawazo ombea fikra zako

Sikio

Mguu

Fikra

Tumbo.

✍️ Inategemea ni eneo gani. Kazi ya damu ya Yesu ni nyingi.

Damu inaongea

Damu inaondoa

Damu inasafisha.

✍️ Kuna mtu alinitumia picha kwenye whatsapp na alikuwa na alama ya kung'atwa na nyoka na meno .lazima unyunyize damu ya Yesu hapo. Na sumu hiyo iondolowe hata kama sio ulimwengu wa mwili basi ulimwengu wa roho .

Damu inakomboa

Damu inazuia

Damu inafungua

3.Kemea roho za kipepo zilizoingia na mifupa ilivyotetemeka.

✍️ Limejifunua kwa picha ipi. Mfano yule wa nyoka kemea pepo la nyoka.

Buibui kemea bui bui au wanyama kemea kila picha ni roho.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Kama usipoona picha angalia kazi iliyofanyika kama unajiona umekufa kemea roho ya mauti.

4. Omba Mungu akuponye maeneo yote yaliyopata madhara kwa kupitia ndoto hiyo.

Mawazo Mungu aponye.

Hofu Mungu aondoe hofu na akupe amani.

Na Mungu atakuponya katika eneo ulilopata shida..

Mwingine aliona nyoka kaingia kwenye biashara na hakumtoa nyoka na baadaa yaa pale business ikafa.

Na mama mmoja aliota ndoto nyoka kapita tumboni kwake na ndoa yake ilipata shida

Na kuna mtu aliotaa mtu kachukua pochi ndogo ndani ya begi na alipoamkaa ile pochi haijarudi. Na alipoenda ofisini alibadikishiwa kazi na alishwa cheo. Yamkini alisema ntaomba kesho na usiku tu kufika asubuhi Tayari mambo yamebadilika

Watu wanaota wanakula vitu na watu waliokufa na zoezi lilifanyika kuombea hali hiyo.

Si kila kula kwenye ndoto ni ishara mbaya.

Unakula na nani wapi saa ngapi na kwa ajili ya nini. Na kama wana israel walikula chakula baada ya kuabudu ndama. Kile kilikuwa ni sakramenti kwa miungu

Utakuta kama wenzi wanataka kukupeleka kwenye agano wanakupeleka kula chakula ambacho hakijakaa vizuri kwenye ndoto ..

Pia unaweza andika ndoto yako na kuituma ili iombewe na utampa mhudumu au andika kwa msg kwa namba za huduma.

Chukua namba hizo na andika ujumbe wa msg kwenda namba hizo kwenye link hii.
<http://www.mwakasege.org/kuchangia.htm>

Au andika barua pepe angalia katika link hii. **<http://www.mwakasege.org/mawasiliano.htm>**

Pia nenda kwenye ukurasa wa Facebook na andika kwenye **inbox**
<https://www.facebook.com/Christopher-Diana-MwakasegeMana-Ministry-132462780111984/>

Hakikisha unampata huyu Yesu hakiisha unaokoka na unakuwa na mahusiano mazuri na Mungu. Wokovu sio dini mpya bali unajenga uhusiano wako na Yesu.

SIKU YA PILI

Kuna mambo 2 ambayo yanaweza kutumika katika NDOTO

JAMBO 1

Shetani anaweza kutumia NDOTO kupandikiza mambo ambayo usipoyang'oa mapema yataharibu maisha yako

JAMBO 2

Kutazama ishara zitakazo kuonyesha kuwa NDOTO zinahitaji kufuatiliwa

ISHARA

1. Kujisikia kufadhaika moyoni kwa ajili ya NDOTO uliyoota

Kufadhaika maana yake ni mahangaiko unayoyapata ndani ya Moyo wako(kuutibua moyo)

Mwanzoni 41:1-8"....8. Hata asubuhi roho yake IKAFAIDHAICA akapeleka watu kuwaita waganga wote wa misri...

▶▶ Usifanye kosa kudharau NDOTO yoyote utakayoota Ukasema kumbe ni ndoto tu, inabidi kuifuatilia
Mwanzo 41. 7 b Basi Farao akaamka , kumbe ni NDOTO tu

Mwanzo 40:5-6 "Wakaota ndoto wote wawili, kila mtu ndoto yake usiku mmoja, kila mtu kwa tafsiri ya ndoto yake, mnyweshaji na mwokaji wa mfalme wa Misri waliofungwa gerezani. Yusufu akawajia asubuhi, akawaona wamefadhaika.

Yusufu aliwaona wote wawili mnyweshaji na mwokaji wote WAMEFADHAICA

▶▶ Mfadhaiko huja kama alarm, maana ukishaitega alarm ikilia lazima ushtuke.

2. Kuota NDOTO hiyo zaidi ya Mara moja au inayofanana na hiyo

▶▶ Mwanzo 41:25-32 Mst 32"... **Na ndoto ya Farao kwa vile ilivyokuja mara mbili, ni kwa sababu neno hilo Mungu amelithibitisha, na Mungu atalitimiza upesi**

Unapoota Mara 2 au zaidi ni kukutaarifu unatakiwa kuifuatilia hiyo NDOTO

Ayubu 33:14-15 Kwa kuwa Mungu hunena mara moja, **Naam, hata mara ya pili, ajapokuwa mtu hajali.** Katika ndoto, katika maono ya usiku, Usingizi mzito uwajiliapo watu, Katika usingizi kitandani;

Usipoifuatilia ndipo Mungu huirudisha Mara ya 2 au zaidi hadi utakapopata ufahamu wakulifanyia kazi

▶▶ Jiulize kama Mungu katumia NDOTO kusema na wewe kwa nini iwe vigumu kuelewa maana yake
Warumi 10:17 Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.

Ukiwa na Neno LA Mungu lazima utaisikia sauti yake.

▶▶ Mfano ukiwa na gari ni vema kujua baadhi ya vitu ili likipata shida uweze kulitengeneza sio lazima kila kitu unapeleka garage. Vivyo hivyo kwa watumishi, sio lazima kila tatizo lako unalipeleka kwa watumishi mengine yatatie mwenyewe Yale unayoona huyawezi ndio yapeleke huko, unapotaka kumweleza **Mtumishi jambo lako sikiliza Amani Ya moyo wako kwanza**

3. Ndoto uliyoota kukutia hofu

Daniel 4:5 na Ayubu 4:12-14

*Nikaota ndoto iliyonitia **hofu**; mawazo niliyokuwa nayo kitandani mwangu, na njozi za kichwa changu, zikanifadhaisha. DAN. 4:5*

*Basi, nililetewa neno kwa siri, Sikio langu likasikia manong'ono yake. Katika mawazo yaliyotoka katika maono ya usiku, Hapo usingizi mzito uwaangukiapo wanadamu. **Hofu** iliniangukia na kutetema, Iliyoitetemesha mifupa yangu yote. AYU. 4:12-14*

4. Ukiwa mambo uliyoota kwenye ndoto yanatokea katika mwili

Ayubu 4:12-16 🖐🖐

Mfano

▶▶ Ukiona umeota ndoto unakemea na ulivyoshtuka bado unakemea(fuatilia)

▶▶ Au ulikuwa unalia kwenye ndoto na umeamka unakuta macho yana machozi pia fuatilia

5. Ndoto kukunyima usingizi

Daniel 2:1 *Hata katika mwaka wa pili wa kumiliki kwake Nebukadreza, Nebukadreza aliota ndoto; na roho yake ikafadhaika, **usingizi wake ukamwacha***

6. Kwa na hamu ya kutaka kujua tafsiri ya hiyo ndoto

Mwanzo 40:7-8,41:7-8 *Akawauliza hao maakida wa Farao, waliokuwa pamoja naye katika kifungo, nyumbani mwa bwana wake, akisema, Mbona nyuso zenu zimekunjamana leo? Wakamwambia, Tumeota ndoto wala hapana awezaye kuifasiri. Yusufu akawaambia, Kufasiri si kazi ya Mungu? Tafadhalini mniambie Kisha hayo masuke membamba saba yakayala yale masuke saba makubwa yaliyojaa. Basi Farao akaamka, kumbe! Ni ndoto tu. Hata asubuhi roho yake ikafadhaika; akapeleka watu kuwaita waganga wote wa Misri, na watu wote wenye hekima walioko. Farao akawahadithia ndoto yake, wala hakuna aliyeweza kumfasiria Farao mambo hayo*

Mstr 8 - alitaka kujua ndoto ile ilimaanisha nini

▶▶ Ndoto ya Farao ilibeba maisha ya miaka 14 ya dunia nzima, kama angepuuzia sijui ingekuwa kwa hiyo miaka 14. Kwa hiyo ule msukumo aliokuwa nao ndio ulisaidia utafsiriwa

7. Ndoto uliyoota kukuletea mahangaiko moyoni mwako juu ya Imani na utumishi ulinao kwa Mungu

Kukizuka katikati yako nabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, Na tuiuate miungu mingine usioijua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa BWANA, Mungu wenu, yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda BWANA, Mungu wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. Tembeeni kwa kumfuata BWANA, Mungu wenu; mcheni na kushika maagizo yake na kuisikia sauti yake, nanyi mtumikieni na kushikamana naye. KUM. 13:1-4

▶▶ Usimwogope mtu Bali mwogope Mungu

▶▶ Usikubali jina au huduma yako ivume kuliko jina la Yesu

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Mfano: Punda aliyembeba Yesu alitembea juu ya nguo kwa sababu tu alikuwa kambeba Yesu lakini baada ya kumshusha Yesu alitembea chini kama kawaida. Dhamani uliyonayo ni kwa sababu unae Yesu ndani yako

8. Ukiona uliyoyaona kwenye ndoto yanapinga au ni tofauti ya mipango uliyonayo

Ayubu 33:14-17 Kwa kuwa Mungu hunena mara moja, Naam, hata mara ya pili, ajapokuwa mtu hajali. Katika ndoto, katika maono ya usiku, Usingizi mzito uwajiliapo watu, Katika usingizi kitandani; Ndipo huyafunua masikio ya watu, Na kuyatia muhuri mafundisho yao, Ili amwondoe mtu katika makusudio yake, Na kumfichia mtu kiburi

▶▶ unaweza kuota ili upangue kile kibaya ambacho kinaweza kutokea mbele, hivyo anapozungumza nawe anakusaidia usijeingia kwenye matatizo Fulani au kukuondoa katika mawazo uliyonayo

9. Kusikia msukumo moyoni wa kusimulia ndoto uliyoota

Mwanzo 37:5-11(Pale Yusuph alipowasimulia ndugu zake ndoto aliyoota)

Mathayo 27:19 Na alipokuwa ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe alimpelekea mjumbe, kumwambia, **Usiwe na neno na yule mwenye haki; kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake.**

▶▶ Unaweza kuota ndoto kwa ajili ya mtu mwingine hivyo pale unapopata msukumo moyoni wa kumwambia we mweleze ila omba hekima, na kibali kutoka kwa ROho Mtakatifu

10. Kusikia msukumo moyoni wa kuandika ndoto uliyoota

Habakuki 2:2-3 *BWANA akanijibu, akasema, landike njozi ukaifanye iwe wazi sana katika vibao, ili aisomaye apate kuisoma kama maji. Maana njozi hii bado ni kwa wakati ulioamriwa, inafanya haraka ili kuufikilia mwisho wake, wala haitasema uongo; ijapokawia, ingojee; kwa kuwa haina budi kuja, haitakawia.*

▶▶ Unaandika kwa sababu unaweza kuisahau asubuhi au kwa ajili ya kufuatilia huko mbeleni

▶▶ Uwe unaandika ndoto zakusaidia baadae

Note: Kama huwa unasahau ndoto unazoota weka daftari na kalamu karibu ili unapoota tu uwe unaziandika na baadae iwe rahisi kuzifuatilia hatua kwa hatua.

11. Ukiwa umesahau ndoto uliyoota ila moyoni unajisikia msukumo wa kutaka kujua

Daniel 2:1-5

Baada ya Nebkadreza kusahau ndoto Daniel alienda kumweleza hiyo ndoto tena

▶▶ Ukiota ukasahau jitahidi kuifuatilia kwani ktk ulimwenngu wa roho imerekodiwa km ile ya Nebukadreza.

MAOMBI

▶▶ Toba kama kuna mojawapo ya ishara hizi 11 hukuzifuatilia(kwa kujua au kutojua) Mungu arudishe hizo

Ndoto ili aseme nasi tena haijalishi muda gani umepita

SIKU YA TATU

Jana tulipitia mambo mawili

JAMBO 1

Shetani anaweza kutumia NDOTO kupandikiza mambo ambayo usipoyang'oa mapema yataharibu maisha yako

JAMBO 2

Kutazama ishara zitakazo kuonyesha kuwa NDOTO zinahitaji kufuatiliwa

Jambo 3

▶▶ Tumia viashiria vilivyokuja na ndoto ili kujua ikiwa umeiombea hiyo Ndoto na kuifuatilia ipasavyo

VIASHIRIA- Imetoka katika Neno ishara

Marko 16:17 **Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;**

▶▶ Ishara haziji peke yake huwa zina ambatanishwa na kitu Fulani

Kutoka 4:1-8Mstr 8... Basi itakuwa, wasipokusadiki, **wala kuisikiliza sauti ya ishara ya kwanza, wataisikiliza sauti ya ishara ya pili.**

▶▶ Ishara zina sauti

Musa aliambiwa kwa ishara ya kijiti kilichokuwa kinaungua bila kuteketea

▶▶ Ishara ilikuwa kama kibao ili kuelekeza kuwa hayo yaliyosemwa ni kweli

▶▶ Ndoto lazima zije na viashiria ili uzifuatilie, ishara ndani yake imebeba msukumo wa kitu fulani

Daniel 4:4-7 *Mimi, Nebukadreza, nalikuwa nikistarehe katika nyumba yangu, nikisitawi katika nyumba yangu ya enzi. Nikaota **ndoto iliyonitia hofu**; mawazo niliyokuwa nayo kitandani mwangu, na njozi za kichwa changu, zikanifadhaisha. **Basi nikatoa amri kwamba wenye hekima wote wa Babeli, waletwe mbele yangu, ili kunijulisha tafsiri ya ndoto ile.** Ndipo wakaingia waganga, na wachawi, na Wakaldayo, na wanajimu; nikawahadithia ile ndoto; wao wasiweze kunijulisha tafsiri yake.*

Katika Ndoto ya Nebukadreza ilibeba mambo 4

1. Hofu

2. Mfadhaiko

3. Msukumo wa kupata tafsiri

4. Msukumo wa kuisumulia

▶▶ Nia ya Nebukadreza ilikuwa ni kutafuta Tafsiri ya hiyo ndoto. Hizo Ishara 4 zilikuja kwa msisitizo ili kumfanya atafute maana yake ndio maana alitafuta watu mbalimbali kumtafsiria

▶▶ Ukiona umeota ina ishara zaidi ya 1 ujue ina mzigo na inabidi uifuatilie

Daniel 4:6-7(hapa aliota ndoto) 🖐🖐

Angalia tena Daniel 20-26(alipewa Tafsiri ya ndoto) *Ule mti uliouona, uliokua, ukawa na nguvu, urefu wake ukafika mpaka mbinguni, na kuonekana kwake mpaka dunia yote. ambao majani yake yalikuwa mazuri, na matunda yake mengi, na ndani yake chakula cha kuwatosha wote.; ambao chini yake wanyama wa kondeni walikaa, na ndege wa angani walikuwa na makao yao katika matawi yake; ni wewe, Ee mfalme, uliyekua, na kupata nguvu; maana ukuu wako umekua na kufika mpaka mbinguni, na mamlaka yako yamefika mpaka mwisho wa dunia.*

Tena, kwa kuwa mfalme alimwona mlinzi, naye ni mtakatifu, akishuka kutoka mbinguni, akisema, Ukateni mti huu, mkauangamize; ila kiacheni kisiki cha shina lake katika ardhi, pamoja na pingu ya chuma na shaba, katika majani mororo ya kondeni. kikatiwe maji kwa umande wa mbinguni, na sehemu yake iwe pamoja na wanyama wa kondeni, hata nyakati saba zipite juu yake; tafsiri yake ni hii. Ee mfalme, nayo ni amri yake Aliye juu, iliyomjia bwana wangu, mfalme; ya kuwa utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni, nawe utalazimishwa kula majani kama ng'ombe, nawe utatiwa maji kwa umande wa mbinguni, na nyakati saba zitapita juu yako; hata utakapojua ya kuwa Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa yeye amtakaye, awaye yote. Na kwa kuwa waliamuru kukiacha kisiki cha shina lake; ufalme wako utakuwa imara kwako, baada ya wewe kujua ya kuwa mbingu ndizo zinazotawala.

27- (alipewa ushauri wa yapi ya kuyafanya)

Kwa sababu hiyo, Ee mfalme, shauri langu lipate kibali kwako; **ukaache dhambi zako kwa kutenda haki, ukaache maovu yako kwa kuwahurumia maskini; huenda ukapata kuzidishiwa siku zako za kukaa raha**

NOTE

▶▶ Watu wengi wanakuwa na hamu ya kutafsiriwa ndoto bila kutaka kusikiliza ushauri uliopo ktk hiyo ndoto

▶▶ Tafsiri ya ndoto ina vitu 2

1. Ujumbe
2. Ushauri

Ni vema uvipate vyote sio kimoja. Nebukadreza alichukua **Tafsiri akaacha ushauri**

Jambo la 3 katika ndoto ya Nebukadreza. Daniel alipata kiashiria kama cha Nebukadreza (mfadhaiko). Daniel alipopewa taarifa ya Ndoto ndani yake ilimtibia

▶▶ Daniel alitaka ajue

1. Yaliyokusudiwa ndani ya Ndoto yatatokea. Mfano kuna watu wanaoota mambo na baada ya muda yanatoka ,usifurahie hizi ndoto huwa ni taarifa ili kama ni mbaya uipangue mapema au kama nzuri uiombee. Una uwezo wa kuibadili Yale yaliyoonekana ktk mst 27

Mst 28".... **Hayo yote yakampata mfalme Nebukadreza...**

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Kama Nebukadreza angefuata ushauri aliopewa na Daniel yasingemkuta hayo kwani alipewa allowance ya miezi 12 ya kutengeneza ila hakuyafuata na baada ya hiyo miezi 12 yakampata ya kukaa kondeni na wanyama miaka 7,

soma Daniel 4:31-33 *Hata neno lile lilipokuwa katika kinywa cha mfalme, sauti ilikuja kutoka mbinguni, ikisema, Ee mfalme Nebukadreza, maneno haya unaambiwa wewe; **Ufalme huu umeondoka kwako. Nawe utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni; utalishwa majani kama ng'ombe, na nyakati saba zitapita juu yako, hata utakapojua ya kuwa Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, awaye yote. Saa iyo hiyo jambo hilo likatimizwa, likampata Nebukadreza; alifukuzwa mbali na wanadamu, akala majani kama ng'ombe, na mwili wake ulilowa maji kwa umande wa mbinguni, hata nywele zake zikakua, zikawa kama manyoya ya tai, na kucha zake kama kucha za ndege.***

☞ Kuna gharama za kupuuzia ushauri unaopewa ,ona yaliyomkuta Nebukadreza aliishia kutolewa ufahamu wake na kuishi porini na wanyama

☞ Ndoto aliyoota kwa muda mfupi aliipuuza kwa miezi 12 na ilimtesa maisha yake kwa miaka 7

☞ Mungu alikiacha kiti cha Nebukadreza kwa miaka 7 bila kiongozi ili ajue kuna Mungu wa mbingu na nchi. Soma Daniel 4: 34-37 *Hata mwisho wa siku hizo, mimi, Nebukadreza, nikainua macho yangu kuelekea mbingu, fahamu zangu zikanirudia. nikamhimidi Yeye aliye juu, nikamsifu na kumheshimu Yeye aishiye milele; kwa maana mamlaka yake ni mamlaka ya milele, na ufalme wake hudumu toka kizazi hata kizazi; na watu wote wanaokaa duniani wamehesabiwa kuwa si kitu, naye hufanya kama atakavyo, katika jeshi la mbinguni, na katika hao wanaokaa duniani; wala hapana awezaye kuuzuia mkono wake, wala kumwuliza, Unafanya nini wewe? Basi wakati uo huo fahamu zangu zikanirudia, na kwa ajili ya utukufu wa ufalme wangu, enzi yangu na fahari yangu zikanirudia; na mawaziri wangu, na madiwani wangu, wakaja kunitafuta; nami nikathibitika katika ufalme wangu, nikaongezewa enzi kupita kiasi. Basi mimi, Nebukadreza, namhimidi Mfalme wa mbinguni, namtukuza na kumheshimu; maana matendo yake yote ni kweli, na njia zake ni za adili; na wale waendao kwa kutakabari, yeye aweza kuwadhili.*

4. Unapo ikumbuka kuifuatilia ndoto mara kwa mara au unapoiombea na ukaona viashiria haviondoki ujue kuna jambo ndani ya ndoto inahitaji kuifuatilia

☞ Mfaidhaiko wa Nebukadreza sio wake ni ndoto aliyoota

☞ Unapopata mzigo wa kumuombea mtu kuombea **ombea saa hiyohiyo** usisubiri kumhadithia mtu hadi upate kibali,unaweza muhadithia ndio ukamvuruga zaidi.

☞ Unaweza kuta umeingizwa kwenye maagano ya ukoo ukawa unaomba bila mafanikio,inabidi ufanye maombi ya kujitoa kwenye hayo maagano kwa kulifuta jina lako kwa Damu ya Yesu ,usiwe kama wale wanaosema **"Ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya"** ni lazima ujitoe kwenye hayo maagano maana huwezi jua wanamtumia mungu gani unajikuta mambo yako hayafanikiwi kumbe umeunganishwa na maagano

Kuna mtu aliota kang'atwa na nyoka ktk ndoto na alivyoamka akajikuta damu inatoka sehemu hiyo. Hivyo alikuwa kaachiwa roho ya mauti na ile sumu iliharibu maisha yake kabisa kwani familia yao ilikuwa imeingia ktk maagano hivyo ingawa alikuwa kaokoka hakufanikiwa kwa sababu yalikuwa na uhalali nae

**SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA
UWANJA WA BARAFU.**

MAOMBI

- ✓ Fanya Toba
- ✓ Ita Damu ya Yesu itakase popote ambapo uling'atwa na ng'e,mbwa,nyoka, mende n.k katika ndoto ili kukuondolea uhalali wa shetani kukutesa
- ✓ Tubu kwa kuachia mlango uliochilia mashambulizi ambayo yanamiliki mwili wako
- ✓ Futa sumu yoyote iliyoachwa kupitia ndoto na ondoa jina lako kwenye maagano kwa kujua au kutojua kwa jina la Yesu

Amen na ubarikiwe sana.

SIKU YA NNE

LENGO: kuhakikisha uhusiano wako na Mungu unaimarishwa, pia tuendelee kumtegemea yeye katika mafanikio

Jambo 1,2 na 3 (tumeyaona kwenye masomi ya siku zilizopita Leo tuendelee na Jambo LA NNE)

JAMBO 4

**IMARISHA IMANI YAKO INAYOHUSU KUTUMIA DAMU YA YESU ILI IKUSAIDIE KUSHUGHULIKIA
NDOTO ZILIZOBEBA VITU VINAVYOKWAMISHA MAISHA YAKO**

▶▶ Tofauti katika kuombea Ndoto ni ile imani uliyonayo kwenye Kutumia Damu ya Yesu

▶▶ Ndoto pia huwa zina vipindi vyake, unapoota ndoto angalia muda uliyoota ndoto hiyo na cheki huwa unaota muda gani. **Kuna vipindi 4 vya muda - SAA 1-3, SAA 4-6, SAA 7-9 na SAA 10-12**

check ndoto zako unaota ktk kipindi gani

Waebrania 11:1, *Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.*

Warumi 10:17 *Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo*

▶▶ Imani chanzo chake ni kusikia sio Neno. Ni lazima usikie kwanza .Unaweza kusikia ila usisikie na unaweza kusikia na usielewe

Yakobo 2:20,26 Lakini wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba **imani pasipo matendo haizai?** Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na **imani pasipo matendo imekufa.**

Unaweza kuwa na Imani na isikusaidie kitu

▶▶ Wakristo wengi wana Imani ya Damu ya Yesu ila wengi hawana Imani katika kuitumia hiyo Damu ya Yesu.

HATUA ZITAKAZOWEZA KUIMARISHA IMANI YAKO

HATUA 1

Uwe na Mistari ya Neno la Mungu katika Biblia juu ya Damu ya Yesu

Kutoka 12:12-13, 21-23

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

*Maana nitapita kati ya nchi ya Misri usiku huo, nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa mwanadamu na wa mnyama; nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri; Mimi ndimi BWANA. *Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lo lote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri. Hapo ndipo Musa akawaita wazee wa Israeli, na kuwaambia, Nendeni, mkajitwalie wana-kondoo kama jamaa zenu zilivyo mkamchinje pasaka. Nanyi twaeni tawi la hisopu, mkalichovye katika ile *damu iliyo bakulini na kukipiga kizingiti cha juu, na miimo miwili ya mlango, kwa hiyo damu iliyo katika bakuli;* tena mtu ye yote miongoni mwenu asitoke mlangoni mwa nyumba yake hata asubuhi. Kwa kuwa BWANA atapita ili awapige hao Wamisri; na *hapo atakapoiona hiyo damu katika kizingiti cha juu*, na katika ile miimo miwili, BWANA atapita juu ya mlango, wala hatamwacha mwenye kuharibu aingie nyumbani mwenu kuwapiga ninyi. KUT. 12:12-13, 21-23*

1 kor 5:7 Basi, jisafisheni, mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana **Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani, Kristo;**

Unapotumia na mstari katika Agano la kale uwe na unaofafana nao katika agano jipya. Tafuta mstari utakaokupa uhalali wa kuitumia katika MAOMBI yako.

HATUA 2

Tafakari hayo maneno   hadi uone ile Waebrania 11:1 na Yakobo 2:20 itokee moyoni mwako (imani na matendo)

▶▶ Mistari ya HATUA ya kwanza ina mambo yatarajiwayo. Mungu aliwaambia wana Wa Israel watapona tu kwa sababu ya Damu ikiwepo juu ya miimo ya mlango yao, nao waliyasikia hayo na kupata uhakika wa kuwa yaliyosemwa yatatokea

Yakobo 2:20

Imani pasipo matendo haizai

▶▶ Suala la kuweka kwenye matendo ni la muhimu sana katika utumiaji wa Damu ya Yesu. Musa nae aliweka kwenye matendo kwa kutii ndio maana hawakuangamizwa (Kutoka 12:21-23) 

HATUA YA 3

Wana wa Israel kushiriki kwa matendo kuitumia Damu ya Pasaka ili Mungu aweze kuitumia kama wao walivyoitumia.

Kumbuka: Mungu haitumii Damu ya Yesu ambayo wewe huitumii ni lazima kwanza uikubali kuitumia ndipo naye ataitumia kama waisrael walivyofanya huko Misri

▶▶ Mungu anatazama Damu uliyoitumia kwanza kwani inaonyesha Imani yako ipoje

▶▶ Mungu hutafuta Damu iliyofanyika Ishara ili yeye naye aone Imani yako

▶▶ Mfano: kuna tofauti ya kupanda bus na kujifunza kuendesha bus, hii itakusaidia hata dereva akishindwa kuendesha wewe unaweza kuendesha.

Hiyo pia ipo ktk utumishi wetu kuna watu wanajua kuombewa tu ila kujiombea hawawezi.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Mfano mwingine ni pale unaponunua simu itategemea unataka kuijua kwa kiwango gani, kama unataka kujua kupiga na kupokea uwezo wako utaishia hapohapo. Hivyo kama una kiu ya kutaka kujua zaidi utajifunza zaidi ili kupanua uelewa wako

▶ Vivyo hivyo kama Damu ya Yesu unaitumia kwa ajili ya kwenda mbinguni tu au kujifunika tu, itaishia kufanya kazi hiyohiyo unayoiamuru, ila kumbuka Damu ya Yesu inatumika popote unapoihitaji alimradi uwe na imani katika kuitumia.

Kumbuka Damu ya Yesu unaweza

👉 kuimwaga,

👉 inanyunyuziwa

👉 pia unaweza kunywa hivyo usikariri kazi moja tu,

▶ Kama hulitumii Jina au Damu ya Yesu jua nae Mungu hatalitumia kwako.

NB:

Kuna walioota wakifanya mapenzi kwenye ndoto, wengine wakifunga ndoa ktk ndoto au unakuta upo kwenye ndoa ila unaota unafanya mapenzi na mke/ mumeo hizo ndoto sio nzuri.

Kwani unakuwa tayari umeingia katika Agano la kwanza katika ulimwengu wa roho. Ndio maana unakuta binti au kijana wanachelewa kupata wenzi kwani wanakuwa tayari wameshaingia Agano ktk ulimwengu wa Roho. Au ndoa INA mafarakano au zinavunjika kwa ajili ya hayo maagano. Hapo inabidi uitumie Damu ya Yesu ili uvunje hilo Agano la kwanza

MAOMBI

▶. Kama umeota hayo 👉👉 shika kitovu chako alafu ingia kwenye:



1.Toba, rehema na utakaso.

Tubu popote ulipoacha mlango hadi hiyo roho ya uzinifu ikaingia kwako, pia Toba kwa ajili ya UOVU wa wazazi wetu vizazi vya nyuma

2. Ondoa Agano la kwanza kwa kutumia Damu ya Yesu

3. Jitenge na huyo uliezini nae ktk ndoto na uliefunga nae ndoto, jitenge na Pete, mavazi, zawadi,nk. kwa Damu ya Yesu

Hapo kwenye sehemu ya

Muombe Mungu akutenge kama alivyowatenga wana Israel na Wamisri na pia alivyowatenga na yule mharibu alieua wazaliwa wa kwanza wa Misri.

4. Pia tulifanya MAOMBI ya kujiweka WAKFU kwa Bwana

- Wakfu Nafsi,mwili na roho

- Uongozwe na Bwana ktk mambo yako

- Usonge mbele kimwili na kiroho
- Utumie mapenzi ya Mungu katika maisha yako na sio akili yako.

 Ubarikiwe sana!!!

SIKU YA TANO

Lengo ni kuimarisha uhusiano na Mungu ili umtegemee na kumtumaini ili akisaidie katika kufanikiwa kwako

Baada ya semina hii Mungu akusaidie kukupa maarifa ya ndoto na uelewe na uweze kuwasaidia na wengine.

Jambo la 5. Vijue vyanzo vya ndoto ili ujue kuviombea ipasavyo.

Ni rahisi kufuatilia na kuombea ndoto ambayo unajua chanzo chake.

1. Chanzo cha kwanza ni Mungu.

14 Kwa kuwa Mungu hunena mara moja, Naam, hata mara ya pili, ajapokuwa mtu hajali. 15 Katika ndoto, katika maono ya usiku, Usingizi mzito uwajiliapo watu, Katika usingizi kitandani; Ayubu 33 :14-15

2. Shetani

*Kukizuka katikati yako nabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia akisema, **Na tuiquate miungu mingine usiyojua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto, kwa kuwa BWANA, Mungu wenu, yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda BWANA, Mungu wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote. Tembeeni kwa kumfuata BWANA, Mungu wenu; mcheni na kushika maagizo yake na kuisikia sauti yake, nanyi mtumikieni na kushikamana naye. KUMBU KUMBU LA TORATI. 13:1-4***

 Haijalishi ndoto ina mbwembwe kiasi gani au ishara kiasi gani kuna zingine sio za Mungu hata kama zinatokea . **Hivyo kuwa makini sana.**

3.Shughuli nyingi

Kwa maana ndoto huja kwa sababu ya shughuli nyingi; na sauti ya mpumbavu kwa njia ya wingi wa maneno. MHUBIRI . 5:3

 ndoto zingine huja kwa sababu ya shughuli nyingi.

4. Hali ya Kiroho ya mahali ulipolala

*Yakobo akatoka Beer-sheba, kwenda Harani. Akafika mahali fulani akakaa huko usiku kucha, maana jua lilikuwa limekuchwa; akatwaa jiwe moja la mahali pale akaliweka chini ya kichwa chake, akalala usingizi pale pale. **Akaota ndoto; na tazama, ngazi imesimamishwa juu ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni. Tena, tazama, malaika wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake. Na tazama, BWANA amesimama juu yake, akasema, Mimi ni BWANA, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka; nchi hii uilalayo nitakupa wewe na uzao wako. Na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya***

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

nchi, nawe utaenea upande wa magharibi, na mashariki, na kaskazini, na kusini; na katika wewe, na katika uzao wako, jamaa zote za dunia watabarikiwa. Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia. Yakobo akaamka katika usingizi wake, akasema, Kweli BWANA yupo mahali hapa, wala mimi sikujua. Naye akaogopa akasema, Mahali hapa panatisha kama nini! Bila shaka, hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo lango la mbinguni. Yakobo akaondoka asubuhi na mapema, akalitwaa lile jiwe aliloliweka chini ya kichwa chake, akalisimamisha kama nguzo, na kumimina mafuta juu yake. Akaita jina la mahali pale Betheli; lakini jina la mji ule hapo kwanza uliitwa Luzu. MWANZO. 28:10-19

☞ lile eneo lilikuwa ni madhabahu ya Mungu hapo mahali alipolala yakobo.

☞ Kujua hivi vyanzo vya ndoto vitakupa mtaji wa kuomba ipasavyo na tutapita kwenye mifano hapa ili kuomba.

1. MFANO WA KWANZA.

NDOTO KUTOKA KWA MUNGU

Kwa kuwa Mungu hunena mara moja, Naam, hata mara ya pili, ajapokuwa mtu hajali. Katika ndoto, katika maono ya usiku, Usingizi mzito uwajiliapo watu, Katika usingizi kitandani; Ndipo huyafunua masikio ya watu, Na kuyatia muhuri mafundisho yao AYUBU. 33:14-16

☞ Omba Mungu akupe neema ya kusikia katika ndoto anazokuletea sio swala la kupuuzia tu ambalo Mungu analisisitiza usifanye bali kuna kitu kipo kwenye hiyo ndoto anataka upate. **Omba Mungu akupe hiyo neema maana hataki upoteze muda katika maisha haya anataka uishi kwa faida.**

☞ Na omba Mungu akupe neema ya kujua kilichobebwa na ndoto. Na anaposema **kufungua masikio** lengo Mungu afungue masikio yako maana mchana unaweza unakwa busy sana husikii akisema na wewe ila usiku anakuja kwa njia ya ndoto ili kuongea na wewe

☞ Omba Mungu akusaidie kusikia kilichoko ndani ya ndoto ili afungue masikio yako ya ndani. Angalia mstari wa 16. Unaoaema kutia muhuri Mafundisho yao.

☞ Kama umepata Mafundisho na hujui kuwa ni ya Mungu atakuja kwenye ndoto kuthibisha au kubatilisha na utajua tu.

Mfano kuna mtu alikuwa kaokoka na anaenda mahali pengine kupata neno la Mungu. Na alienda mahali hapo mara kwa mara na mwishoni akaamua **moyoni** kuhamia hapo ili awe anasali hapo hapo. Na usiku aliota ndoto Mchungaji wa mahali hapo anawaongoza watu kwenda porini na wakapotea njia. Na yeye alikuwa anaowaona.

Na alipoamka usingizini, alielewa maana yake nini lakini ni baada ya kupita katika shule hii ya ndoto **akajua kuwa kuwa Mungu amkataza asihamie pale.**

Na angalia 17 Ili amwondoe mtu **katika makusudio yake, Na kumfichia mtu kiburi; Ayubu 33 :17**

☞ alikuwa anamtoa kwenye makusudi yake ya kutaka kuhama kanisa.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

✍ Na usipuuzie ndoto unazoota na Mungu alinisukuma kulifuatilia somo la ndoto kwa sababu Mungu alisema nami kwa mambo mengi kwa ndoto.

✍ Siku nataka kuacha kazi kabla ya wakati maana wito uliwaka sana ndani na hali hii unaweza dhani wengine wanatania yaani hawafanyi kazi ya Mungu ila wewe ndio utafanya. Elia alisema nimebaki peke yangu Mungu alimwambia kuwa wapo watu 7000 Kwa hiyo usiwaze kuwa wewe tu ndio mtenda kazi. *Lakini ile jawabu ya Mungu yamwambiaje? Nimejisazia watu elfu saba wasiopiga goti mbele ya Baali. Warumi 11:4*

✍ Basi niliona watu ng'ambo wako kwenye senyenge (uzio) na kuna mto mkubwa na mimi niko upande mmoja. Akaja mtu mweusi ananiambia ruka ruka. Nikasema ngoja nitafute pa kupitia.

Nikamwambia ngoja nione pa kupita nikaona mwamba nikasema si umeona nikapata kupitia. Na **nilipoamka Roho mtakatifu akiniambia kuwa hiyo pressure ya kuacha kazi sio yangu**. Tulia hadi upate pa kukanyaga.

Hivyo inahitaji utulivu katika huduma.

2. MFANO WA PILI (NDOTO KUTOKA KWA MUNGU)

Mwanzo 41. Farao alipoota ndoto za njaa na ndoto zile haikuwa kwa taarifa tu, bali ilikuwa na maelezo ya kipindi cha maandalizi ya kuweka akiba.

✍ Na angepuuzia ina maana dunia nzima na yeye mwenyewe angepata hasara ya kukumbwa na njaa kali bila ya kuwa na chakula.. na ndio maana Mungu aliweka ishara.

Maisha ya Yesu alipokuwa mdogo yamefuatiliwa na ndoto. Yusufu alipotaka kumuacha Mariam na Mungu alisema nae kwa ndoto ili asimuahe. Wakati nawaza namna ya kumuacha Malaika akaongea nae. Na Yusufu alikubali kuendelea na Mariam. maana haikuwa rahisi kuamini kuwa mimba ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu.

*Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema, Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia. Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye. Kisha Herode akawaita wale mamajusi faraghani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota. **Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.**MATHAYO . 2:1-3, 7, 12*

Na ilipita muda Herode alijua kadanganywa.

Na hao walipokwisha kwenda zao, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto, akasema, Ondoka, umchukue mtoto na mama yake, ukimbilie Misri, ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize. Akaondoka akamchukua mtoto na mama yake usiku, akaenda zake Misri; MATHAYO. 2:13-14

*Hata alipofariki Herode, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto huko Misri, akasema, Ondoka, umchukue mtoto na mamaye, ushike njia kwenda nchi ya Israeli; kwa maana wamekufa walioitafuta roho ya mtoto. Akaondoka akamchukua mtoto na mamaye, akafika nchi ya Israeli. Lakini aliposikia ya kwamba Arkelao anamiliki huko Uyahudi mahali pa Herode babaye, aliogopa kwenda huko; ? **naye akiisha kuonywa katika ndoto, akasafiri pande za Galilaya, akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na manabii, Ataitwa Mnazorayo** MATHAYO. 2:19-23*

☞ Kama angepuuzia ndoto hizo Yusufu ingekuwa hasara sana na hata historia ya Ukristo isingekuwa kama ilivyo.. hivyo ndoto itakusaidia kupata utulivu ndani na hutapata mahangaiko ambayo sio ya lazima kuyapata kama ukafuata ndoto ambayo Mungu kaitumia kusema na wewe.

☞ **Mungu alisema nami mengi kwa njia ya ndoto.**

Niliota niko eneo la kijijini eneo la migomba na kuna mtu alinipeleka pale na kulikuwa na kanisa. Na mchungaji wa pale kila akihubiri waumini wa pale wanakufa. Na akatoka na mimi niliingia na hapo kanisa lote watu wamekufa na yule mtu kanipa nguo nyeupe na mimi nikavaa na nikaanza kufundisha watu wakaamka wote na mara 3 kwa theluthi.

Na nikaamka kutoka usingizini na nilijua mambo yafuatayo.

✠ 1. Nilijua wito wangu ni kwa ajili ya kanisa na kuwa kwamua mahali walipokwama.. **ndio maana utaona. Mafundisho ya kukwamua mahali walipokwama.**

3. Mfano wa ndoto Kutoka kwa shetani una iombeaje?

☞ Ziba lango la ndoto ili lisipitishe mambo/ndoto ya shetani maana za shetani ndoto zake zinakuharibu.

*Kutoka 12:21-23. Nanyi twaeni tawi la hisopu, mkalichovye katika ile damu iliyo bakulini na kukipiga kizingiti cha juu, na miimo miwili ya mlango, kwa hiyo damu iliyo katika bakuli; tena mtu ye yote miongoni mwenu asitoke mlangoni mwa nyumba yake hata asubuhi. Kwa kuwa BWANA atapita ili awapige hao Wamisri; na hapo atakapoiona hiyo damu katika kizingiti cha juu, na katika ile miimo miwili, BWANA atapita juu ya mlango, **wala hatamwacha mwenye kuharibu aingie nyumbani mwenu kuwapiga ninyi.***

☞ Waliziba kwa damu ule mlango, ndio maana aliwaambia waweke damu katika vizingiti vya miimo ya malango.

Muhimu. Damu inatumika kuziba mlango na omba. Kwa damu ya Yesu Kristo **nafunga mlango shetani asipitishe ndoto zake. Omba mara kwa mara.**

- ❖ Mungu hatumii damu iliyopo kwenye bakuli ambayo haitumiki. Weka neno kwenye matendo kwa upande wako na yeye anafanya kwa upande wake.
- ❖ Ombea na wototo wako na semea neno eneo la ndoto.
- ❖ Ombea watu na ombea sana watoto ili shetani asipitishe vitu vyake. Na kuanza kupitisha ombea sana hili jambo.

Yule dada niliyekueleza jana kuwa anazini na mtu kwenye ndoto na alikuwa anaomba lakini hali ilimtesa sana na aliponishirikisha na nilipoomba kwa damu ya Yesu zile ndoto zilikoma.

Na endelea kusoma maeneo yanayohusu damu ya Yesu ili imani yako ijenge na Kristo ni pasaka wetu na damu yake inaziba huo mlango.. hii ni siri sana unahitaji kujua..

4. NDOTO ZINAZOKUJA KWA SABABU YA SHUGULI NYINGI UNAIOMBEAJE

Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu zake; naye alipokuwa akizipanda, nyingine zilianguka karibu na njia, zikakanyagwa, ndege wa angani wakazila. Nyingine zikaanguka penye mwamba; zilipoanza kumea zikakauka kwa kukosa rutuba. Nyingine zikaanguka kati ya miiba, na miiba ikamea pamoja

**SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA
UWANJA WA BARAFU.**

*nazo ikazisonga. **Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote LUKA. 8:5-7, 14***

Shughuli nyingi maana yake kutumia muda bila kufuata mapenzi ya Mungu. Yesu alisema sifanyi neno ila lile baba analofanya na alisema anafanya ili kuitimiza kazi yake aliyemtuma aifanye.

Haya sio kwa ajili ya Yesu tu bali hata wewe.. (tangu sasa hatumtabui mtu kwa ajili ya mwili ina maana Yesu akiwa ndani yako unafanana nae...kwa ajili yake yeye.. tumesulubiwa pamoja na Kristo.. Yesu alisema mimi ni mzabibu nanyi ni matawi kwa hiyo sisi ni wamoja na Kristo

Yesu anataka tuzae matunda anayotaka.. matunda yapate kukaa.. matunda yake yanayotokana na mbegu maana Mungu ndiye akuzae hizo mbegu. Na anakuja kuona kama kila mwaka kama kuna mtu ana matunda na kama huzai Mungu anasema huyu akatwe maana hana faida.

Mungu hatazami maisha bali anaangalia matunda kila siku .wiki mwezi.. Mungu anangalia matunda ya muda aliokupa.

*Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisema, Andika, Heri wafu wafao katika Bwana tangu sasa. Naam, asema Roho, wapate kupumzika baada ya taabu zao; **kwa kuwa matendo yao yafuatana nao.** Ufunuo wa Yohana 14:13*

🔑 Mungu atakusaidia na anangalia na kuwa je unafanya kazi aliyokupa?.. na kuna wapendwa wapo kwenye miiba..

🔑📖 Omba Mungu maisha yako yasikae kwenye **miimba**.. miimba imekuja kwa ajili ya adhabu.. jifuze kutembea katika toba..

Omba toba Kama mahali hukufika kiwango Mungu akusamehe fanya hilo kila wakati

Aliyeko kwenye miimba hazalishi kitu na maana kuna mahangaiko huko kasome kwenye biblia. Maana yake kuna watu hawataki wakuzunguke na akasema kaa nao mbali lakini wewe unawang'ang'ania..

*Lakini kama hamtaki kuwafukuza wenyeji wa nchi watoke mbele yenu; ndipo hao ambao mtakaowasaza watakuwa kama sindano machoni mwenu, na kama **miiba ubavuni mwenu**, nao watawasumbua katika hiyo nchi ambayo mwakaa. Hesabu-Numbers 33:55*

🔑 Kama marafiki hawakusaidii kaa nao mbali fika ng'ambo nyingine ndipo watumie kamba kaa nao mbali

🔑 Huwa nawaambia wanafunzi usikae na watu ambao hawasomi.. na wengine wanasema hela ya baba ipo kama hujui alipataje.. maana urithi tosha ni kukuambia kuwa alipate huo utajiri.. au mali.. maana mali ni fikra bila fikta nzuri utakuwa masikini.lazima ujue namna ya kutengeneza hela.

*Ikawa katika kuenenda kwao aliingia katika kijiji kimoja; mwanamke mmoja jina lake Martha akamkaribisha nyumbani kwake. Naye alikuwa na umbu lake aitwaye Mariamu, aliyeketi miguuni pake Yesu, akasikiliza maneno yake. Lakini Martha alikuwa **akihangaika kwa utumishi mwingi**; akamwendea, akasema, Bwana, huoni vibaya hivyo ndugu yangu alivyoniacha nitumike peke yangu? Basi mwambie anisaidie. Bwana akajibu akamwambia, Martha, Martha, unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi; lakini kinatakiwa kitu kimoja tu; na Mariamu amelichagua fungu lililo jema, ambalo hataondolewa. LUKA. 10:38-42*

🔑 Maneno magumu sana na fikiria unachacharika kumtumikia Yesu na anasema unapoteza muda.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

☞ na nilipojua hili jambo niliomba Mungu anisaidie nisitumike kwa hasara.

☞ Unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya utumishi mwingi na unapomtumika Mungu cheki una utulivu kiasi gani na usihangaike na usifurahie unavyomaliza kilomita je unakimbia kwenye utumishi wa kwako.

☞ Unajua kwanini Yesu hakuenda kumponya Lazaro, lakini yeye aliona baba yake aliona kuwa anamfufua japo alipelekewa taarifa kwa emergence lakini hakwenda. hadi alipokufa ndipo alienda ku

☞ Yohana 17 Yesu anasema kazi uliyonipa nimemaliza na kama alimaliza kazi mbona dodoma hajafika **alifanya alichotumwa kufanya** na lengo kubwa la Yesu kuja sio kuponya wagonjwa tu wa wakati ule bali ni kufa msalabani maana kwenye msalaba ndiko kuna ukombozi mkubwa.

Mungu anatafuta vipaumbele na huna muda wa kufanya kila kitu. Na hakuna mwalimu atakaye fundisha kila kitu

Na Mungu hawezi kukupa kufundisha kila kitu. Sasa wewe unafundisha hesabu unataka kufundisha na physics na wewe ndio utanata uonekane kuwa wewe njio wewe mtalaam na unajiamini wewe mwenyewe.

Na ninapoandaa semina kama hivi huwa nasikia watu wakisema fundisha na hili na hili huwa nasema nasubiri **Mwalimu mkuu (Roho Mtakatifu) ndiye anipangie kipindi**

Na nikisema namwaga zege najua kabisa shetani hawezi bomoa kazi ya mtu itapimwa.. na jenge ili Yesu akija kupima kazi yangu itakuaje.

☞ Huwa nawauliza wenzangu Yesu akija wakati tunajenga hema anatafuta nini, na kati kati ya semina anangalia nini au baada ya semina

Na jion na asubuh omba Mungu akuongoze hatua kwa hatua.. na usifurahie njia bali hatua ambazo Mungu atakupeleka bali cheki hatu zako.

Hatua za mtu zaimarishwa na Bwana, Naye aipenda njia yake. Zaburi 37:23

Uzielekeze hatua zangu kwa neno lako, Uovu usije ukanimiliki. Zaburi 119:133

☞ Na mbinguni utaenda na utumishi sahau kama hutacheke hatua zako vizuri

Omba Mungu akusaidie...

Ndoto kwa shughuli nyingi zitakuonesha na watu uliokwama nao na Mungu anasema kaa nao mbali.. na omba kwa Mungu usilale kwenye adhabu.. omba toba na Mungu analisamehe tu..

Hamna sababu ya kulala kwenye adhabu wakati damu ya Yesu ipo.. na shughuli nyingi zinakusaidia nini?

Anasa za dunia hii ni vile vitu vinakuvuta na sio vya Mungu kwako enenda sawa sawa na wenye haki.

Mtu yoyote aliyoko kwenye utumishi na kijana aliyeoa mtu na vitu visivyo vyake atajua tu..

☞ Kuna mahali ukiniona utashtuka na utanishangaa mimi na na utasema na Mwakasege yuko hapa.. na kwa sababu ya nafasi niliyonayo kwa hiyo kuna mahali huwezi nikuta kabisa.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Omba kwa Mungu vipaumbele vya kwako.. na vipaumbele vyangu na mke wangu havifanani nae ana nafasi yake na huwa tuna ombeana na huyu abebe hiki na huyu abebe hiki.

5. MAZINGIRA YA KIROHO UNAOMBEAJE?

Mambo 4 muhimu

1. Ombea chumba unacholala funika kwa damu ya Yesu. Kama ni hotel omba toba kwa kila kilichofanyika nje ya mapenzi ya Mungu.

☞ Nguo zinabeba roho ombea mashuka kwa damu ya Yesu.

Nilikiwa nchi moja na nilifika kwenye hotel moja huko na kuna mtu alikuwa anatufuatilia kila hotel tunayolala..na alikuwa analala baada ya sisi kutoka

Na akawa anasema nawahi upako, je nikalala nalia usiku kucha na yeye atalia

☞ Ombea nyumba nzima.. na ombea ardhi unayolala..na kama kuna madhabahu nyingine na ombea hili jambo mara kwa mara.

☞ Mtu mmoja alipita kwenye Ardhi anasikia vitu vinagonga chini...

☞ Na mwingine aliomba Mungu naomba ardhi kama imebeba kitu kicho cha kwako.. na akasema naomba itapike kila kitu hapo na akatoka nyoka. Hivi ni vitu vya kweli

☞ Ombea mbingu iliyoko juu maana ina sauti ya kiroho.. na Yesu alipotoka juu ya maji na mbingu zilifunika zina siri ya ajabu sana.. mbingu zinatatandaza utukufu wa Bwana.

☞ Ombea watu wanaoingia mahali hapo Tamari alipobakwa alienda mahali kwa kaka yake.. na ukiwa wa Tamari ulimshika kaka yake ulileta hasira ya kuua. Ukiwa unaua hali ya kiroho.. omba Kama Ayubu.. aliwaombea watoto toba watoto wake.

☞ Kama ni mgeni amekuja kwakoomba kwa ajili yake na vichujwe vitu alivyokuja navyo.. na ombea hili jambo.

Kama unaombea nyumba yako hata kama mtu anavuta sigara hiyo hamu itaondoka akiwa kwako.. na omba sana hivi vitu.

☞ Ni vitu vya kawaida kabisa na anakuja mtu kuwatembelea nyumbani na mnaanza kuota ndoto ngumu ngumu.

Walikuja watu kuniona na mtoto wakasema kuna vitu vinaruka.. na wakasema kuna vitu vinaruka na kumpiga mtoto. Na walisema mama mkwe amekuja nyumbani, na alikuja na mambo yake. Na niliwaambia kuwa either mumuwekee kikao au mwombee rehema kwa Mungu na usione aibu. Mweleze ukweli.

☞ Mtoto mmoja katoka shule kafundishwa hadi kwenda kuzimu na anataka kugeuza chumba chao kuwa kama lango la kuzimu. Na ujue hamtalala salama.

Funika macho yako tuombe

wimbo wa nisalama rohoni

SIKU YA SITA

Kama hukuwepo hakikisha unapata kanda na tumekwenda hatua kwa hatua. Sikiliza na sikiliza itakusaidia sana..

tembelea www.mwakasege.org kupata malelezo namna ya kupata kanda.

The One Year [®] Bible

<http://bible.com/r/y> (Plan ya kusoma biblia kwa mwaka mmoja)

Pdf za masomo;

<https://drive.google.com/folderview?id=0BxdP6mgDJWByUIBweWJhNWxOSUE>

Jambo la sita

YAJUE MAENEO MUHIMU YATAKAYO KUSAIDIA KATIKA KUFASILI NDOTO.

🔗 **LENGO LA SOMO:** Kuimarisha uhusiano wako na Mungu katika Kristo Yesu. Na usiishie kujua tu mambo ya ndoto bali uhusiano wako na Mungu uimarike.

🔗 Katika biblia unaona Yusufu na Daniel wakifasili ndoto. Sasa sio mara zote utakutana na Yusufu au Daniel lakini ndoto utaendelea kuota hiyo. Kwa hiyo fahamu wewe mwenyewe kwa kuomba Mungu na akupe ufahamu wa kufasili ndoto na kumjua Mungu katika Kristo Yesu.

🔗 Maeneo haya yanafanya kazi pamoja.

ENEO LA 1.UWE NA KIU YA KUTAKA MUNGU AKUSAIDIE KUJUA TAFSIRI YA NDOTO HIYO.

*Wakamwambia, Tumeota ndoto wala hapana awezaye kuifasiri. Yusufu akawaambia, **Kufasiri si kazi ya Mungu? Tafadhalini mniambie** MWANZO. 40:8*

🔗 kufasili ndoto ni kazi ya Mungu. Kwa hiyo na wewe jua kufasiri ndoto ni jukumu la Mungu na wewe weka Imani yako kwa Mungu ili afasiri ndoto yako

*Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, **Yesu akasimama, akapaza sauti yake akisema, Mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe.** Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa. YOHANA. 7:37-39*

Kila aliye na kiu aende kwa Yesu na sio kwa mtumishi. Japo Mungu anaweza kukufungulia mlango wa kwenda kwa mtumishi hakikisha unamtukuza Mungu. Na hakikisha imani yako hakikisha imani yako inaenda kwa Mungu.

Pia kuwa Mwangalifu na watumishi **Kumbu kumbu 13:1-4** inasema kuna watumishi wanamtumikia **mungu** lakini sio **Mungu** wa Kwako yaani katika Kristo Yesu. *Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho. Maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu. Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyaifasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.1 WAKORINTHO. 2:10, 13*

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

☞ Ndoto inakupata picha ya vitu vilivyoko Katika ulimwengu wa Roho mwenyeji wetu ni Roho Mtakatifu.

☞ Hakikisha unakuwa na **kiu ya kutosha**

Hapa nakufundisha namna ya kuonesha kiu kwa Mungu.

*Basi Danieli akaingia, akamwomba mfalme ampe muda, kisha yeye atamwonyesha mfalme tafsiri ile. Ndipo Danieli akaenda nyumbani kwake, akawapasha habari kina Hanania, na Mishaeli, na Azaria wenzake; ili waombe rehema kwa Mungu wa mbinguni kwa habari ya siri hiyo, ili kwamba Danieli na wenzake wasiangamizwe pamoja na wenye hekima wa Babeli. **Ndipo Danieli alipofunuliwa siri hiyo katika njozi ya usiku. Basi Danieli akamhimidi Mungu wa mbinguni.**DANIEL. 2:16-19*

☞ Nabukedreza aliota ndoto na alisahau na aliita watu wote wakaldayo na wachawi na wenye hekima.

☞ Na waliposhindwa kumkumbusha ndoto yake alitangaza kuwaua wote. Na taarifa alipelekewa Daniel. Na Daneil aliomba Kwa Mungu na akampa ile ndoto na tafsiri yake.

Namna ya kuwa na Kiu

1. Tenga muda wa kuombea hiyo ndoto kwa msukumo

Maana ilikuwa ni ngumu kwao wasingeshughulikia ile ndoto ya mfalme kwa maana Mungu wao asingejibu maombi yao wangeuawa.

☞ Weka msukumo ndani yako wa kutaka kuombea na weka msisitizo ndani yako ya kuomba na ndio maana **Yesu alisema kila aliye na kiu aje kwangu**. Na Roho Mtakatifu anajua siri za Mungu na atakupa kujua.

Tenga muda wa kuombea ndoto

☞ Masomo kama haya yanakusaidia usipuuzie ndoto maana Farao alitaka kupuuzia ndio maana akisema kumbe ni **ndoto tu** alidharau na alitaka kuiacha.

Kile kiashiria kilimpa kumbana na alitafuta tafsiri. Kwa hiyo unapoota ndoto mahali pa kwanza ni **kwenda kwenye maombi**.

Ndoto ikikuondolea usingizi ombea muda huo huo. Mke wa Pilato alipewa muda mfupi na hakuomba kuhusu mateso ya Yesu na hakuomba *Na alipokuwa ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe alimpelekea mjumbe, kumwambia, Usiwe na neno na yule mwenye haki; **kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake.**Mathayo 27:19*

Ukiota ndoto na unaomba kwenye ndoto endelea kuomba na wewe kama umeshtuka kutoka usingizini hiyo ni ishara ya hiyo ndoti inahitaji kushughulikiwa saa hiyo.

ENEO LA 2.UWE NA NENO LA KUTOSHA LA BIBLIA MOYONI MWAKO ILI USIKIE MUNGU AKISEMA NA WEWE

Kuna hekima ya Mungu, na mwanadamu na shetani. Maana yake kwa hekima yote **tumia neno la Mungu kwa hekima ya Mungu ili Mungu apate utukufu**.

Uwe na utaratibu wa kujijaza neno la Mungu la Kutosha moyoni mwako.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Kwa sababu Ayubu 33:14-15 14 Kwa kuwa Mungu hunena mara moja, Naam, hata mara ya pili, ajapokuwa mtu hajali. 15 Katika ndoto, katika maono ya usiku, Usingizi mzito uwajiliapo watu, Katika usingiziy kitandani;

Mungu anasema kwa ndoto kwa mambo mengi..

Warumi 10:17 Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa **neni la Kristo**.

Zaburi 103:20 20 Mhimidini Bwana, enyi malaika zake, Ninyi mlio hodari, **mtendao neno lake, Mkiisikiliza sauti ya neno lake**

☞ Ndoto ni neno katika picha. Hii ni tafsiri nyingine.. maana ya kwanza nilikuambia kiwa ndoto ni picha ktk ulimwengu wa Roho.

Kwa hiyo kama huna neno la Mungu huwezi kuelewa na kusikia huja kwa neno la Kristo kwa hiyo ili upate ujumbe unahitaji neno.

Ndani yako kama una kiu lazima Mungu atasema na wewe na kukuhimiza ujaze neno lake.

Hivi umewahi jiuliza kwanini hujasoma biblia yote. Maana usisingizie muda kwa sababu uko mda mwingi online whatsapp na kwenye mitandao na unasema huna muda. Kwani waatumishi wanajuaje kwa sababu wanasoma neno.

Weka utaratibu soma sura 3 agano la kale na 1 agano jipya kila siku utamaliza. Au nenda kwenye simu yako weka utaratibu wa kusoma biblia mara moja kwa mwaka.

☞ Naona mtu anaota ndoto yuko chini ya mlima na unazungua huo mlima na hujajua maana yake.

Biblia inasemaje kuzunguka mlima huu umetosha.

Nilivyouzunguka mlima huu vyatosha; geukeni upande wa kaskazini. Kumbukumbu la Torati 2:3

Mungu anasema saa yako ya kutoka imefika lakini hujajua kwa sababu huna neno la kutosha.

Ndoto zingine zina ujumbe moja kwa moja

Nilipokuwa chuo SUA (wakati ule ilikuwa Faculty of Agriculture chini ya chuo Kikuu cha Dar es Salaam) Morogoro nikaota ndoto niko ndani na ikaja karatasi nyeupe ikashushwa na kunyanyuliwa juu mara tatu. Na nilishindwa kusoma na ukaja ujumbe na sauti ikasema hiki ni kitabu cha Joshua .

Na kumbuka nilikuwa sijaokoka nikamwambia Marehemu baba yangu na alisema Mungu anakumbia somakitabu cha Joshua .

Baada ya mwaka kupitia nilipokuwa nakarabia kuokoka na nikaona katika macho haya na nikaonesha kitabu cha Joshua tena

Na nikaonesha na historia na Mungu akisema nani atakaye poka koleo ya Musa . Na nguvu za Mungu zilinishukia na nikawa nanena kwa lugha nikijua naumwa nimeanza kuchangangikiwa maana nilikuwa sijui kitu cha kunena kwa lugha.

Kwa hiyo nikafunga mdomo lakini huku ndani (moyoni) nasikia Bwana Yesu asifiwe.

Nilijua hapa nimechanganyikiwa.. marehemu mama alikuwa anawahi kuja kunitazama maana alijua saa yoyote nakufa kwa namna nilivyokuwa naumwa

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Na baba yangu nilipomueleza alisema Mungu kasema na wewe mwaka jana kwenye kitabu cha Joshua soma na sasa anakuuita kuanza kazi.

*2 Musa mtumishi wangu amekufa; **haya basi, ondoka**,vuka mto huu wa Yordani; wewe na watu hawa wote, mkaende hata nchi niwapayo wana wa Israeli. Yoshua 1 :2*

Na baba yangu alisema rudi chumbani kwako kaongee na Mungu niliokoka mwenyewe kitandani kwangu na si kuongozwa na mtu na nilikuja hata sijui nini maana ya sala ya toba na Mungu alinisaidia na **nikaweka agano na Mungu kuwa sitaenda kuhubiri bila uwepo wake.**

Na baada ya hapo nikasoma tena kitabu cha Joshua na nikapata ujumbe na kitu cha kifanya.

Habari za Nebukadreza .. alitaka tafsiri na hakutafuta ujumbe. Usifanye kosa hilo la **kufurahia tafsiri ya ndoto na kuacha ujumbe..** si siuala la kusoma neno tu bali hakikisha unapata unachotafuta.

Kama ni uponyaji utaona uponyaji.. nuru neno ni taa litakuongoza, hakikisha unapata kitu cha kukusaidia katika neno.

Nimeona watu wanatafsiriana ndoto na unaona hawako sahihi.. na nagundua kuwa hawana neno la kutosha.

ENEO LA 3. Omba Mungu akupe ufahamu wa kudumu juu ya ndoto

*17 Basi, kwa habari za hao vijana wanne, Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; **Danielii naye alikuwa na ufahamu katika maono yote, na ndoto. Danieli 1 :17***

Paulo aliwaombea waefeso ufahamu

*Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, **awape ninyi roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye;18 macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; Waefeso 1 :17- 18***

Na usiombe kujumla omba specific kuwa Mungu naomba ufahamu wa kufahamu ndoto.

Mungu anahamu ya wewe uwe na ufahamu maana yeye ndiye aliyetengeza hiyo njia ya kuwasiliana na wewe kwa ndoto

*6 Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao. **Waebrania 11 :6** 1 Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. **Waebrania 11 :1***

*17 Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo. **Warumi 10 :17***

Mungu ni mzazi anataka aongee na wewe kwa lugha ya kawaida. Kama wewe hukai na watoto wako atajua sana ile lugha ya ya mlezi wake kama ni hause girl au house boy au bibi. Na ndio maana Mungu anataka kukupa njia ya kudumu ya kusema na wewe maana ni mzazi wako

Tokea Mungu ananifundisha jambo hili naona moja kwa moj ndoto nyingi sana.mimi naona urahisi kwa sababu niliamua kujifunza lugha ya Mungu ya ndoto.

Kama Mungu alisema na mimi kwaa njia ya ndoto na kama nilielewa basi ujue na wewe atakusaidia.

ENEO LA 4. Kumbuka ulichokuwa unawaza au kukiombea kabla ya ndoto

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

20 aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; Waefeso 1 :20

☞ Mungu anajibu ndoto na mawazo yako

*18 Kuzaliwa kwake Yesu Kristo kulikuwa hivi. Mariamu mama yake alipokuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. 19 Naye Yusufu, mumewe, kwa vile alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri. 20 **Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema, Yusufu, mwana wa Daudi, kumchukua Mariamu mkeo, maana mimba yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. 21 Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao. 22 Hayo yote yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema, 23 Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake Imanueli; Yaani, Mungu pamoja nasi. 24 Naye Yusufu alipoamka katika usingizi, alifanya kama malaika wa Bwana alivyomwagiza; akamchukua mkewe; Mathayo 1 :18-24***

Ina maana alikuwa anawaza kumwacha Mariam na Mungu alijibu moja kwa moja na angalia 16 Ndipo huyafunua masikio ya watu, Na kuyatia muhuri mafundisho yao **17 Ili amwondoe mtu katika makusudio yake**, Na kumfichia mtu kiburi; **18 Yeye huizua nafsi yake isiende shimoni, Na uhai wake usiangamie kwa upanga. Ayubu 33 :18**

☞ Kagua ulikuwa unawaza nini na hiki ndicho unakipata kwenye Mathayo _Kisha Herode akawaita wale mamajusi faraghani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota. Akawapeleka Bethlehemu, akasema, Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie. Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtolea tunu; dhahabu na uvumba na manemane. **Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine. MATHAYO . 2:7-8, 11-12**

Na Mungu aliwaonya walipotoka tu kwa Herode kwa njia ya ndoto na Mungu aliwakataza. Kitu cha muhimu kwenye ndoto ni ujumbe. Maana hatujaambiwa ndoto hapa ila ni *ujumbe ndio muhimu*.

Nebukadreza alipotukuka na alimsahau Mungu na aliota ndoto na akaona mti mkubwa.. na ndege wapo hapo na aliona mlinzi akija kuuagiza mti ukatwe na Daniel akaja kumfasiria na alifadhaika moyoni na yeye.

Na Daniel alimwambia

Ndipo Danieli, aliyeitwa jina lake Belteshaza, akashangaa kwa muda, na fikira zake zikamfadhaisha. Mfalme akajibu akasema, Ee Belteshaza, ndoto ile isikufadhaishe wala tafsiri yake. Belteshaza akajibu, akasema, **Bwana wangu, ndoto hii iwapate wao wakuchukiao, na tafsiri yake iwapate adui zako.** ni wewe, Ee mfalme, uliyekua, na kupata nguvu; maana ukuu wako umekua na kufika mpaka mbinguni, na mamlaka yako yamefika mpaka mwisho wa dunia. ya kuwa utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni, nawe utalazimishwa kula majani kama ng'ombe, nawe utatiwa maji kwa umande wa mbinguni, na nyakati saba zitapita juu yako; hata utakapojua ya kuwa Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa yeye amtakaye, awaye yote. **Hayo yote yakampata mfalme Nebukadreza. Baada ya miezi kumi na miwili, alikuwa akitembea ndani ya jumba la kifalme katika Babeli. Hata neno lile lilipokuwa katika kinywa cha mfalme, sauti ilikuja kutoka mbinguni, ikisema, Ee mfalme Nebukadreza, maneno haya**

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

unaambiwa wewe; Ufalme huu umeondoka kwako. Nawe utafukuzwa mbali na wanadamu, na makao yako yatakuwa pamoja na wanyama wa kondeni; utalishwa majani kama ng'ombe, na nyakati saba zitapita juu yako, hata utakapojua ya kuwa Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, awaye yote. **Saa iyo hiyo jambo hilo likatimizwa, likampata Nebukadreza; alifukuzwa mbali na wanadamu, akala majani kama ng'ombe, na mwili wake ulilowa maji kwa umande wa mbinguni, hata nywele zake zikakua, zikawa kama manyoya ya tai, na kucha zake kama kucha za ndege.** DANIEL. 4:19, 22-22, 25, 28-29, 31-33

Na amri ya walinzi ilikuja na kumundoa kwenye nafasi yake na alisema tengeza mambo yako na Mungu **Kwa sababu hiyo, Ee mfalme, shauri langu lipate kibali kwako; ukaache dhambi zako kwa kutenda haki, ukaache maovu yako kwa kuwahurumia maskini; huenda ukapata kuzidishiwa siku zako za kukaa raha.**DANIEL. 4:27

☞ Na yote yalitokea baada ya miezi 12. ☞ **Na hakujali na alipewe tafsiri na ujumbe**

ENEO LA 5. IKIWA UMEOTA NDOTO NA UMESAHAU OMBA MUNGU AKUKUMBUSHE. NA AKUPE TAFSIRI YAKE NA UJUMBE.

Daniel 2:1-29. Nabukadreza aliota ndoto na alisahau. Ndani yake alisahau kabisa. Wachawi nao walisahau. Akina Daniel waliomba kwa Mungu awakumbushe na walipewa na tafsiri yake na ndoto aliyoota.

Na nebukdreza hakubisha maana alikumbushwa yote.

☞ Kuna miaka kadhaa mama yangu alikuwa anasumbuliwa jambo fulan na kitu kilichokuwa kina namsumbua nilishuhuduwiwa kuwa kuna ndoto aliota lakini nilipomuuliza alisahau. Na niliomba na Mungu alimkumbusha na nilijua namna ya kuombea.

Kama Mungu anaweza zuia usisahau mwombe Mungu usisahau kwa sababu ulisahau kuomba ili usisahau.

Omba Mungu akusaidie.. na ndio maana andika ndoto zako. Hakikisha unaandika ndoto andika wakati huo huo.

Na ukiota ndoto na ukawa unakumbuka kijumla itakupa shida kutafsiri na wengine wameandika wamesoma shule uliyoota. Sio sawa uko chuo kikuu unaota uko primary au kindergarten.

Hakikisha cheki akina nani wanakuzunguka na ni nani na mtihani huo ni nini kesho tutapita..

Na kesho ntaanza kukufundisha namna ya kutumia vipengele fulani fulani.

📖 **Maombi:** Hakikisha unaokoka na Mungu anakuia uoko msalaba ni kwa ajili yako na Roho Mtakatifu afungue mlango wa Kuokoka maana kuokoka sio dini mpya bali ni kuhamishwa kutoka ufalme wa giza kwenda ufalme wa mwana wa Pendo lake.

Mapepo yote achia watu hawa tunafuta laana zote za ukoo na kila kinachozuia usiokoke kwa damu ya Yesu Mungu wafungulie mlango kama Seth na muokoke . Na Mungu mpe neema ya wokovu mtu anayesoma somo hiki katika Kristo Yesu.

☞ Nazungumza na wewe kama hujaokoka na unatamka huyu Yesu. **Au ulirudi nyuma njoo kwa Yesu na neema ipo rudi kwa Yesu.**

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Soma sala hii

Sala ya Toba*

 Inawezekana kabisa ya kuwa wewe unayesoma ujumbe huu hujaokoka - yaani hujampokea Yesu Kristo ndani ya moyo wako kama Bwana na Mwokozi wako. Lakini sasa umeona umuhimu wa kumpokea Yesu Kristo katika maisha yako.

Naamini Roho Mtakatifu ameweka fursa hii mikononi mwako kwa mpango maalum wa Mungu ili ufike mahali pa kutubu na kuokoka. Inawezekana kabisa, pia ya kuwa hujawahi kuambiwa juu ya umuhimu wa wewe kuokoka. Lakini napenda kukuambia ya kuwa ni mpango wa Mungu uokoke. Soma Wakolosai 1:13,14 na Yohana 1:12-14 na 1 Timotheo 2:3-6 na Warumi 1:16,17 na Yohana 3:7. Ni vigumu kuona baraka za Damu ya Yesu bila ya kuokoka.

Kwa hiyo kama unataka kuokoka - tafuta mahali palipo na utulivu, na usome kwa sauti sala ifuatayo: **(ukiweza unaweza kupiga magoti unapoomba sala hii)**

"Ee Mungu wangu ulie Mtakatifu. Ninakuja mbele zako. Mimi ni mwenye dhambi. Naomba unisamehe dhambi zangu zote nilizokukosea katika maisha yangu. Ninatubu kweli. Naomba damu ya Yesu Kristo iliyomwagika msalabani kwa ajili yangu initakase sasa katika roho yangu na nafsi yangu na mwili wangu. Nimefungua moyo wangu. Bwana Yesu Kristo nakukaribisha ndani yangu. Ingia kwa uwezo wa Roho wako – uwe Bwana na Mwokozi wangu kuanzia sasa na siku zote. Ahsante kwa kunisamehe na kwa kuniokoa. Nimejitoa kwako nikutumikie katika siku zote za maisha yangu. Shetani hana mamlaka tena juu yangu katika jina la Yesu Kristo. Amina.

Ikiwa umesoma sala hii kwa kukusudia kabisa na kwa imani, basi wewe umeokoka na dhambi zako zimesamehewa na kusahuliwa na Mungu sawasawa na alivyoandika katika neno lake. Damu ya Yesu iko juu yako sasa.

Baada ya kuokoka

Unapoanza maisha haya mapya katika Yesu Kristo nakushauri mambo yafuatayo:

1. Zungumza na Mungu kwa maombi kila siku (Yohana 15:7)
2. Soma Neno la Mungu (Biblia) kila siku (Matendo ya Mitume 17:11)
3. Mruhusu Roho Mtakatifu akutawale (Wagalatia 5:16-25; Warumi 8:14-17)
4. Umtumaini Mungu kwa kila jambo katika maisha yako (1Petro 5:7; Zekaria 4:6)
5. Usiache kukusanyika na kushirikiana na wengine waliompokea Yesu Kristo kuwa Mwokozi wao kama wewe ili uimarike zaidi (Waebrania 10:25)
6. Soma jarida la "Hongera kwa Kuokoka." 

Ukipenda unaweza kuniandikia kwa anwani yangu <http://www.mwakasege.org/mawasiliano.htm> juu ya uamuzi uliofikia leo wa kuokoka, ili tumshukuru Mungu pamoja, na tuzidi kukuombea; na pia, tukutumie maandiko mengine ya kukusaidia:

Soma kitabu cha Hongera kwa kuokoka katika maandishi haya

<http://www.mwakasege.org/mafundisho/hongera/utangulizi.htm>

SIFA NA UTUKUFU NI KWA YESU

SIKU YA SABA

Jana tulianza kuangalia jambo la sita. Na endelea kufuatilia somo hili kwenye ukurasa wa Facebook. Christopher & Diana Mwakasege (Mana ministry). <https://www.facebook.com/Christopher-Diana-MwakasegeMana-Ministry-132462780111984/>

Pia tuombe tutayarisha kitabu cha Ndoto kibiblia. Na kikiwa tayari tutawapa.

Summary.

YAJUE MAENEO MUHIMU YATAKAYOKUSAIDIA KUTAFSIRI/KUFASIRI NDOTO

1. Uwe na kiu ya kutaka Mungu akusaidie kujua tafsiri ya ndoto hiyo.

Mwanzo 40:8 Mwenye kufasiri ndoto ni Mungu. Hata Daniel alisema hivyo.

2. uwe na neno la biblia la kutosha moyoni mwako ili uweze kusikia ujumbe uliomo katika ndoto.

Warumi 10:17 Kusikia huja kwa neno la Kristo na Wakolosai 3 inasema neno la Kristo na likae kwa wingi moyoni mwako kwa hekima yote.

3. Omba Mungu akupe ufahamu wa kudumu juu ndoto.

Daniel alikuwa na ufahamu wa mambo yote. Na wewe omba. Ombeni nanyi mtapewa.

4. Kumbuka ukichokuwa unawaza/kuombea kabla ya kuota ndoto.

Waefeso 3:20 Mungu anajibu mawazo yako.

5. Ikiwa umeota ndoto na umesahau omba Mungu akukumbushe.

Daniel 2:1-29. Daniel aliomba Mungu na akamkumbusha ndoto ya Nebukadreza.

LEO TUNAENDA NDANI KUANGALIA ZILE NDOTO AMBAZO WATU WAKO SHULE AU CHUO

☞ Hata kama hujawahi kuota daka sana hili somo. Na utapa maarifa ya kumsaidia mtu mwingine

Mfalme akamwambia Ashpenazi, mkuu wa matowashi wake, awaleta baadhi ya wana wa Israeli, wa uzao wa kifalme, na wa uzao wa kiungwana; vijana wasio na mawaa, wazuri wa uso, wajuzi wa hekima, werevu kwa sababu ya maarifa yao, wenye kufahamu elimu, watakaoweza kusimama katika jumba la mfalme; tena alimwambia awafundishe elimu ya Wakaldayo, na lugha yao. Huyo mfalme akawaagizia posho ya chakula cha mfalme, na ya divai aliyokunywa, akaagiza walishwe hivyo muda wa miaka mitatu; ili kwamba hatimaye wasimame mbele ya mfalme. DANIEL. 1:3-5_

☞ Iko siri ya ajabu sana kwa watu wanaoota wako shule au chuo katika habari hii ya Daniel

1. UKIOTA UKO SHULENI AU CHUONI MAANA YAKE NI

☞ Hatua iliyoko mbele yako inahitaji maandalizi ya fikra zako yanahitaji utaratibu maalumu

**SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA
UWANJA WA BARAFU.**

tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo; Yaangalieni yaliyo mbele ya macho yenu. Mtu akijitumainia mwenyewe ya kuwa ni mtu wa Kristo, na afikiri hivi pia nafsiini mwake, ya kwamba kama yeye alivyo mtu wa Kristo, vivyo hivyo na sisi 2 KOR. 10:5, 7

Maana aonavyo nafsiini mwake, ndivyo alivyo. Akuambia, Haya, kula, kunywa; Lakini moyo wake hauwi pamoja nawe. **MITHALI. 23:7 SUV**

kwa maana yeye ni aina ya mtu ambaye kila mara anafikiri juu ya gharama. Anakuambia, “Kula na kunywa,” lakini moyo wake hauko pamoja nawe. **Mithali 23:7 NEN**

CHUO ni sehemu ya maandilizi na huwa unaandaliwa kifikra. Na maandalizi ya watu kifikra upo kwenye mfumo wa elimu. Na biblia inasema Fikiri.

Katika kiingereza

For as **he thinks in his heart, so is he**. As one who reckons, he says to you, eat and drink, yet his heart is not with you [but is grudging the cost]. Proverbs 23:7 AMPC

for he is like one who is inwardly calculating. "Eat and drink!" he says to you, but his heart is not with you. Proverbs 23:7 ESV

For as he thinketh in his heart, so is he: Eat and drink, saith he to thee; but his heart is not with thee. Proverbs 23:7 KJV

For as he thinks within himself, so is he. “Eat and drink”, he says to you, but his heart is not with you. Proverbs 23:7 TLV

🔑 Alivyo kimtazamo ndivyo alivyo, ulivyo ni matokeo ya misimamo yako ya kifikra uliyonayo. **Maisha yako hayabadilishwi na cheti, bali ni misimamo yako kifikra.**

Kuna mfumo rasmi huu unaitwa mfumo wa Elimu na biblia inaita elimu ya ufalme wa Mungu. Na shetani anataka kupinga na kuweka wa kwake.

Lakini haina maana ya watu wasiosoma na wana maisha mazuri maana kuna watu wemeishia darasa la saba lakini wana maisha mazuri kuliko watu wa degree 3. **Maana maisha sio cheti ni fikra.**

Mungu anaongea na wewe kukuambia kuwaa kuna hata uko mbele.. na akili ziko kwenye nafsi yako. Katika nafsi kuna nia, maamuzi na akili.

Ayubu 33:14-15 Mungu husema na mtu kwenye ndoto na hajali na 16. Anafungua masikio yake 17 anasema kumuondoa kwenye makusudio yako.

Unakuta mtu anaomba Mungu naomba nisaidie hatua iliyoko mbele yangu na Mungu anakuletea ndoto ya shule. Ina maana kuna hatua iliyoko mbele yako inahitaji maandalizi.

Au uko katikati ya maandilizi na Mungu anakuletea ndoto ya shule na anakumbia hapo uko shule.. akina Daniel waliwekwa shule miaka 3 kwa ajili ya maandalizi. Sasa ingekuwa ni kosa kwao kutafuta kazi baada ya mwaka mmoja. Na kama wangukuwa wanaomba Mungu awape kazi uwe na uhakika angewaleta ndoto ya kuwa wako shule au chuo.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

✍ Ina maana kuna hatua iliyoko mbele mbele yao. Na hii inawapata sana hawa watumishi ambao moto wa kumtumikia Mungu unawaka sana ndani yao. Na Mungu wakiwa katika hali ya namna hiyo Mungu anawaletea ndoto ya kuwa wako chuo. Hapo inamaanisha kuwa ni sehemu ya maandalizi. Kaa hapo vumilia hapo ulipo maana saa yako bado.

✍ Pia Mungu anasema na wewe kuwa maandalizi ya hatua inayokuja huwezi kujiandaa ipasavyo peke yako. Na ina maana huwezi jisomea peke yako na nenda shule ili uandaliwe.

2.KAMA UNAOTA NA CHUO AU SHULE ULIYOSOMA ZAMANI MAANA YAKE NINI.

✍ Ina maana ya kwamba kuna jambo fulani ulitakiwa kuvuka hapo kifika lakini hukuweza kuvuka. Na kwa sababu hiyo kuna eneo kwenye maisha yako limekwama kwa sababu hiyo.

Ndio maana nilikuambia lazima ujifunze kuhusu ndoto ili uulize na ujifunze zaidi. Kwa hiyo kama huelewi uliza kwa Mungu na fuatilia kwenye biblia .

3. KUOTA UKO PRIMARY (SHULE YA MSINGI)

✍ Haijalishi uko wapi na ume ota uko shule ya msingi. Maana yake fikra za kimsingi yaani foundation za kufikiri kuna kitu ulikosa kwenye msingi wa kufikiri.

Sasa unakuta wewe unaomba kwa ajili ya kuingia kwenye ndoa au kupanda cheo lakini unajikuta unaota ndoto uko primary.

✍ Mungu anzungumza na wewe juu ya misingi yako mizuri ya maamuzi na wewe hujaandaliwa bado/hauko vizuri. Biblia inazungumza juu ya maamuzi na inasema "amani ya Kristo iamue moyoni mwako"

Ndio maana waalimu wanaofundisha shule ya msingi na mwalimu akakosea kumuwekea msingi mwanafunzi wa kupenda shule ataharibu kabisa maisha yake.

Na sasa watu wengi wanatarajia masomo ya msingi yapelekwe awali lakini si kila mtoto atapata nafasi ya kwenda awali. Lakini mfumo rasmi unahitaji uendele darasa la kwanza na ndiko kuna foundation ya kufikiri kwako maana ndipo inajengwa hapo.

Waalimu wa darasa la kwanza na la pili ni muhimu sana maana ndio msingi wamaisha ya wengi. Mwalimu ukipewa hiyo nafasi chungu sana.

Mama yangu alikuwa mwalimu na kafundisha miaka yote lakini alifundisha darasa la kwanza na la Pili na alikuwa mwalimu mkuu.

Sasa watu wengi Mungu anawapa ndoto za kuwa wako primary hata kama wamemaliza chuo kikuu. Na hapo Mungu anasema na wewe kuwa misingi yako ya kimaamuzi, kihisia au makusidio hayako vizuri. Kwa hiyo unahitaji kwenda kwa Mungu ili akusaidie ujue hiyo misingi.

4.JE WALE WATU ULIO NAO DARASANI KATIKA NDOTO.

✍ Ina maana kuwa hao ni watu mlio nao ngazi moja ya kimaandalizi.

5.UKIOTA NDOTO UKO DARASANI NA WATU ULIOWAHI KUSOMA NAO ZAMANI

✍ Maana yake kuna eneo mlikwama kifika kwa kufanana ina maana kuna maandalizi unahitaji kufanya. Wewe fanya utafiti utakuta na wewe umekwama hapo.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Kwa hiyo Mungu anasema na wewe kuwa unahitaji kuvuka hapo.

6. UKIOTA HUKAI DARASANI NA UNATEGEA AU UNATOROKA.

🏠 Maana yake huna utulivu unaotakiwa kuwa nao ili uweze kujiandaa au kuandaliwa kwa ajili ya hatua inayokuja.

Au unaomba Mungu akupe kujua kwanini umekwama hapo unakuta Mungu anaongea na wewe kwa njia hii ili kukuonesha kuwa ulikuwa unatega shule aliyokuwa anakuandaa.

Mtu anayetega darasani anakuwa na maisha mabovu. Maana kuna baadhi ya chuo usipohudhuria masaa kadhaa wanakudiaqualify. Maana hamna namna nyingine ya kuweza kuelewa kama hukai darasani.

Kwa wale waalimu kama mimi wanaelewa maana yake nini hapa. **Maana nazungumza na wewe lisaa limoja kila siku. Na huwa natumia masaa 4 au matano au siku 2 au tatu kabla na unasema na kufundisha lisaa limoja.**

Huwezi fanya maandalizi ya dakika 5 alafu uongee masaa 2. Kwa Mungu muda wa maandalizi ni muhimu sana kuliko muda wa kufanya kazi. Sasa jaribu tegea shule alafu tafuta kazi. Ujue huwezi pata. Kwa hiyo tafuta utulivu mbele ya Bwana.

Kuna vitu vinaweza kukuondolea utulivu kama miradi, marafiki, au maisha haya.. ndio maana kusoma shule ukubwani ni shida. Au ni mazingira nayo yanakukosesha utulivu.

Nadhani mlisikia msiba wa mama yangu uliotokea Dar es Salaam. Na tulikuwa familia na nipo katikati ya semina. Na Mungu alitupa kufanya maamuzi na kujua na gharama yake. Sasa tulichagua kuendelea na semina na **halikuwa jambo jepesi. Na kwa mara ya kwanza ndio nilielewa kwanini mtu akifiwa huwa anazungukwa na watu.** Na niliwahi fiwa lakini sikuwahi kukutana hali hiyo.

Na wenzangu wanaliponiuliza niliwaambia kuwa tutaendelea na semina. Na wadogo zangu nao wakasema kaka tuko pamoja na tukagawana majukumu na tukatawaanyika kila mtu eneo lake. Hapo ilikuwa ni masaa 7 tu tokea mama kafariki. Na jion semina inanisubiri. Sasa wote wameondoka na nimebaki peke yangu ili kuandaa semina na hicho ndio kilikuwa kipindi kigumu kwangu sana.

Maana ghafla picha ya mama yangu dk za mwisho ilikuja na naona madaktari wamemzunguka na mmoja akaja kuniambia Mwakasege mama hayupo na kila nikitazama ile picha yake. Niliona wakiandika death certificate. Na walisema ngoja tukaweke mwili mortuary na tuliusindikiza.

Na nilipofungua biblia sikuona maandiko ya biblia nilikuwa naona picha ya mama yangu, na nilianza kuwaza maamuzi haya kuwa sasa kama sina utulivu wa ujumbe kutoka kwa Mungu sasa ndio ntaenda kuhubiri kitu gani.

Kwaa mara ya kwanza nilielewa kwanini unazungukwa na watu ukifiwa maana niliona mara ya kwanza tulikuwa na watu wametuzunguka na uchungu uliisha pale maana si watu walikuwepo.

Nikafunga biblia na nikaanza kuomba kwa kunena kwa lugha, maana kwa mazingira ya namna hiyo huwezi kuomba kwa kiswahili. Maana nakumbuka nilipokuwa nazungumza na wenzangu. Walisema Mwakasege sio swala la kuhubiri bali ni kuwa utaweza. Na niliwaambia niinulieni watu wa kuniombea. Na baada ya muda baada ya kuomba nguvu za Mungu zilinishukia na ghafla nikapata utulivu kama sina msiba vile. *Mkono wa Mungu ulinyamazisha kila kitu.*

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Na ujumbe ukaja na nilikaa lisaa lizima na niliandika na nilipokuwa nimeenda kufundisha nilikuwa nafundisha kama sijafiwaa vile. Hata watu wengine walikuwa wanasema inawezekana hatujasikia sawa sawa maana sidhani kama amefiwa.

Nataka kukuambia kuwa kwa **Mungu kuwa utulivu ni muhimu maana hata Martha na Mariam walikuwa na shida hiyo**. Yesu alisema huyu aliyetulia ndiye kachagua fungu jema.

7. UKIOTA UNASOMA NA UKAONA SOMO UNALOSOMA.

☞ Maana yake Mungu anasema na wewe juu ya aina na eneo unalohitaji kujiandaa vizuri kifika.

8. UKIOTA UNAJINDAA KUFANYA MTIHANI AU UNAFANYA MTIHANI.

☞ Maana yake unapimwa kiwango chako ulichofikia kimaandalizi. Ulichofikia kimaandalizi kama unaqualify kwenda hatua nyingine.

Hili unaliona pale ambapo akina Daniel walipewa mtihani wa kitaifa. Na ulitungwa na Nebukadreza na alisaisha mwenyewe. **Na wa nne tu ndio waliofaulu.**

Kazi ya mtihani sio kupima tu masomo yako bali ni kucheki kama uko tayari kwa kilichoko mbele yako.

Ndio maana usifurahie tu kufaulu mtihani, bali faulu maisha kwa kutumia masomo.

Biblia haisemi kwenye lugha walipata ngapi, bali biblia inasema hivi waandaliwe ili waweze kusimama kwenye ikulu ya mfalme, na wanne ndio walionekana wanafaa kusimama mbele ya mfalme na haisemi ndio waliofaulu masomo yao.

Wakati nilipokuwa nazungumza na watoto wangu wakiwa primary. Nilizungumza nao sentensi hii na iliwashatua kidogo nilipowaambia kuwa **si suala la kufaulu mtihani bali ni kufaulu maisha**. Na kama mkifaulu tu mtihani na mkakwama maisha ina maana sikuwekeza vizuri kwenye maisha yenu. Kwa hiyo ninacho tafuta ni kufaulu maisha na mtihani. Na hili suala sio jepesi maana wengi wanataka kufaulu masomo tu. Na sio kufaulu maisha.

Na utashangaa hufaulu maisha, na ulikuwa hujiandai kufanya kazi na ulikuwa unajindaa kufaulu mtihani. **Unafaulu mtihani lakini maisha umekwama.**

☞ Na fuatilia na hilo somo ulilooneshwa.

10. UKIOTA UNAFANYA MTIHANI NA UMEFELI.

☞ Hujafikia kiwango ambacho ulikuwa unatakiwa. Kwa hiyo huaminiki kwenda hatua inayofuata.

11. UKIOTA UKO SHULE AU CHUO NA UKIOA KITU KINACHOHUSIANA NA MAMBO YA KIROHO.

☞ Mwingine anaota yuko darasani na kuna biblia. Na anauona nyoka, mjesi au bibi yake na aliyekufa au unamuona mchungaji kavalia rasmi.

☞ Ukiona namna hiyo ina maana kuna jambo la kiroho limetokea ukiwa shule na linakusumbua mpaka sasa. Mungu aliwaambia akina Daniel kuwa chakula na vinywaji havikuwa vizuri rohoni. Na lazima vyakula vilikuwa vinatolewa sadaka.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Na walijua kabisa hali ya kiroho ingeweza haribu maandalizi yao. Hali ya kiroho ilijotokeza mwanzoni kabisa wakati wanaanza maandalizi ya masomo yao ya miaka 3.

Baada ya miaka 3 walionekana kuwa mara 10 zaid kuliko wachawi wale waliokiwa wame wazunguka.

Huyu ndugu alikuwa na wachawi na alikuwa anawataka kuwaondoa kazini, aliwatafuta watu wengine na ndio maana alikuwa anataka kuona je wanafiti kiasi gani.

Maana hamna haja ya kuondoa watu wazuri kazini na ukaleta watu ambao si bora kuliko hao. Ujue tu utendaji wa kazi utakwenda chini.

Na kilicho wasababisha kuwa wawe mara kumi bora ina maana ni kitu cha kiroho kilichokuwa chuoni. Na ilikuwa ni chakula. Na ndio maana Mungu aliwazuia kula.

12. UKIOTA UKO SHULE AU CHUO NA UKO ENEO LA CHAKULA (DINING AU CAFETERIA)

☞ Kama ni hivyo ombea chakula ulichokula au kitu kilichogusa fikra zako. Maana utashangaa kuwa ulipokuwa unakula kumbe kuna vitu mlizungumza na vikapandwa na viliharibu maisha yako.

Kwa hiyo kila ukiomba Mungu akuvushe unaonesha hapo ombea ulichokula shule.

Tulikuwa mkoa mmoja hapa nchini kwenye mkutano kama huu na niliona katika ulimwengu wa Roho watu wana mavazi marefu na wanafuatilizia watoto na wanawapa chakula watoto chakula si kizuri. Mungu aliniambia futa hiyo kitu kwenye damu yao maana kinashika fikra zao.

Na nilitangaza kufuta kwa damu ya Yesu. Na kulikuwa na mapepo mengi sana yalilipuka na Mungu alinionesha wazi wazi lakini anaweza sema na wewe kwa njia ya ndoto.

13. UKIOTA UKO SHULE AU CHUO NA UMEMALIZA COURSE NA HUPATI KAZI NA UKIOMBA MUNGU UPATE KAZI UNAOTA UKO SHULE.

☞ Maana yake ni hii kuna shida kati ya kitu ulichosoma na soko la ajira unalotafuta kazi. Kwa hiyo lazima uombe Mungu aunganishe kati ya ulichosoma na soko la ajira.

Kuna watu walisoma miaka 3 na akina Daniel na hawana kazi kwa sababu masomo yao ilikuwa ni kwa ajili ya kukaa ikulu ya Nebukadreza . Na hawana kazi.

Omba kwa Mungu ili akusaidie kusoma masomo yatakayohitajika na soko la ajira. usisome masomo ambayo soko lake linabadilika na unasoma sasa na baada ya miaka 3 imejaa watu. Na unaanza kukemea shetani.

Hamna mfumo wa Elimu unao fundisha watu saa hiyo hiyo au muda huo huo waingie kazini. **Ikitokea wanaita crash program au inservice training.**

Lakini kama ni kwa ajili ya miaka 5 utashangaa hata hawahangaiki kupata kazi maana ajira zao zinakuwa tayari (demanded)

Miaka ile tunasoma sisi tulikuwa tunaletewa barua kabisa chuoni hata kabla ya kumaliza. Na barua ya kwanza ilikuwa ni National Insurance Corporation. Lakini sikuenda huko. Maana nilienda kufanya kazi nyingine.

Hii ni dondoo kwa uchache.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

MAMBO YA KUFANYA SASA

1. Omba toba kwa Mungu kama kuna mahali hujufanya vizuri wakati wa maandalizi.
2. Omba Mungu akuvushe.

Na mtu mmoja alidaka na alianza kuomba na alisema Mwalimu ulipofundisha nilikuwa naota ndoto niko tu primary na nilianza kuomba na kuomba na niliomba Mungu aniasidie.

Baada ya muda kadhaa niko chuo na niliendelea kuvuka hatua kwa hatua. Na nilimwambie endelea kuvuka

USIKUBALI FIKRA ZAKO ZIKWAME OMBA KWA MUNGU

Mungu atakusaidia kwenda darasani au atakupata Vitabu. Fanya kitu ambacho Mungu atakupata.

Niliona mahali katika shule ya seminary sista yuko form one na watoto wadogo nae anasoma.

Kwa hiyo fuata maelezo Mungu atakayokupa.

Ubarikiwe.

SIKU YA NANE

Lengo: Kuimarisha uhusiano wako na Mungu ili ufanikiwe kimaisha.

Ndoto ni njia ambayo Mungu anaitumia kuongea na mtu, na kwa wakati ule wetu ilikuwa shida sana kupata masomo haya ya ndoto. Kwa hiyo hii ni neema kusikia masomo haya kwa wakati huu. Tafsiri za ndoto zipo kwenye biblia kwa hiyo fuatilia hatua kwa hatua.

Na nilikuambia tunaandika kitabu cha Ndoto na tunaomba Mungu atusaidie kitoke mwaka huu.

Summary

Kwa kuwa Mungu husema, wakati huu kwa njia moja, au wakati mwingine kwa njia nyingine, ingawa mwanadamu anaweza asielewe. Mungu husema na mwanadamu katika ndoto, katika maono ya usiku, wakati usingizi mzito uwaangukiapo wanadamu wasinziapo vitandani mwao, Ayubu 33:14-15 NEN

📖 Ndoto ni njia ambayo Mungu anatumia ili uweze kusikia kitu ambacho Mungu anataka kukuambia

*Ikawa, mwisho wa miaka miwili mizima, Farao akaota ndoto; na tazama, amesimama kando ya mto. Na tazama, ng'ombe saba wazuri, wanono, walipanda kutoka mtoni, wakajilisha manyasini. Na tazama, ng'ombe saba wengine wakapanda nyuma yao kutoka mtoni, wabaya, wamekonda, wakasimama karibu na wale ng'ombe wengine ukingoni mwa mto. Kisha hao ng'ombe wabaya waliokonda wakawala wale ng'ombe saba wazuri, wanono. Basi Farao akaamka. Akalala, akaota ndoto mara ya pili. Tazama, masuke saba yalimea katika bua moja, makubwa, mema. Na tazama, masuke saba membamba, yamekaushwa na upepo wa mashariki, yakatokeza baada yao. Kisha hayo masuke membamba saba yakayala yale masuke saba makubwa yaliyojaa. *Basi Farao akaamka, kumbe! Ni ndoto tu*. MWANZO. 41:1-7 SUV*

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

☞ Farao aliposema kumbe ni ndoto tu ina maana alikuwa anataka kudharau. Na naamini wewe sasa hutaweza kudharau ndoto kwa sababu kuna umuhumu mkubwa sana kuifuatilia .

Na ndoto zina vyanzo mbali mbali japo Mungu anaweza tafsiri ndoto zote.

1. Mungu

2. Shetani

3 Shuguli nyingi unapokosa vipaumbele vya kutumia muda vizuri unakuwa na shughuli nyingi maana yake hazina mpangilio

4. Hali ya Kiroho ya mahali unapolala.

Mungu ndiye aliyetengeneza lango la ndoto na kwa kuwa hatujui namna ya kulinda shetani nae analitumia. Na nilikufundisha kuwa linalindwa kwa kwa damu ya Yesu. Ndio inatumika kuziba lango la ndoto

Kama hukuwepo hakikisha unapata kanda na sikiliza itakusaidia sana.

Jana nilipitia baadhi ya ndoto na nyingi sana ni ndoto za shule. Na jana nilikupa mtaji wa kuanzia kufanya maombi

UMUHIMU WA KUFANYA MAOMBI YA KUONDOA KINACHO KUFUATILIA KWA NJIA YA A NDO TOKA KWENYE ENEO UNALOLALA AU ULILOWAHI KULALA

1. SEHEMU YA KWANZA

KUTOKA ENEO UNALOLALA.

Nyumbani kwako, hotelini, kazi, nyumba ulipanga

*akobo akatoka Beer-sheba, kwenda Harani. Akafika mahali fulani akakaa huko usiku kucha, maana jua lilikuwa limekuchwa; akatwaa jiwe moja la mahali pale akaliweka chini ya kichwa chake, akalala usingizi pale pale. **Akaota ndoto; na tazama, ngazi imesimamishwa juu ya nchi, na ncha yake yafika mbinguni. Tena, tazama, malaika wa Mungu wanapanda, na kushuka juu yake. Na tazama, BWANA amesimama juu yake, akasema, Mimi ni BWANA, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa Isaka; nchi hii uilalayo nitakupa wewe na uzao wako. Na uzao wako utakuwa kama mavumbi ya nchi, nawe utaenea upande wa magharibi, na mashariki, na kaskazini, na kusini; na katika wewe, na katika uzao wako, jamaa zote za dunia watabarikiwa. Na tazama, mimi nipo pamoja nawe, nitakulinda kila uendako, nami nitakuleta tena mpaka nchi hii, kwa maana sitakuacha, hata nitakapokufanyia hayo niliyokuambia. Yakobo akaamka katika usingizi wake, akasema, Kweli BWANA yupo mahali hapa, wala mimi sikujua. Naye akaogopa akasema, Mahali hapa panatisha kama nini! Bila shaka, hapa ni nyumba ya Mungu, napo ndipo lango la mbinguni.*** MWANZO. 28:10-17 SUV

Yakobo alipolala na aliota ndoto na kazi ya ile ndoto ilikuwa na kazi kubwa ya kumtaarifu juu ya mahali alipolala.

Na Mungu alikuwa anajitambulisha kwake na ndio maana yako alisema hapa ni nyumba ya Mungu. Ina maana mahali pale palikuwa uwepo wa Mungu.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Jambo lingine ni lango ina maana kuna vitu vya kiroho vinapita pale kutoka katika ulimwengu wa roho kuja ulimwengu wa mwili.

Tulikuwa mkoa mmoja na tulikuwa tunajenga hema, na kuna watu walikuja na wakasema hapa mnapojenga hema mnakata network zetu. Na walisema tutaona nikasema haisha shida. Na tulijua kabisa ni wachawi.

Baada ya siku 2 mchawi wa kwanza aliokoka na wakaenda kutafuta mchawi mwingine mkubwa maana na wao wana ngazi zao.

Jumamosi alikuja kupambana na sisi. Alijaribu kila kitu na alishindwa na akarudi nyumbani kwake, pia Nyumbani kwake kulikuwa na bango ambalo linaonesha kuwa mganga wa kienyeji.

Na alikuwa na uwezo wa kujigeuza umbo lolote na anaingia chumbani kwake na anafungua hata Ardhi. Na alishangaa aliporudi nyumbani kwake alijaribu kila kitu alishindwa.

Na ilibaki moja na alikuwa na kadi ya ATM, na alikuwa anatumia kila mahali maana alipewa kuzimu. Na alipewa masharti kuwa hela atakayochukua lazima aitumie yote. Sasa jumapili alipoenda benki kutoa hela kadi yake ilimezwa.

Na aliona sasa kapatikana alinyoosha moja kwa moja uwanjani aliwakuta wenzangu na alijitambulisha kuwa anaenda kijisalimisha kuwa anataka kuokoka. Na wakamhoji maswali na walienda nae nyumbani kwake.

Na walienda nae nyumbani kwake, na gari kutoka uwanjani huku zinapiga nyimbo za injili na wateja wake walishangaa kuona mganga anakuja na nyimbo za injili maana pale kwake walikuwepo watu waliokuwa wana mahitaji mbali mbali na wamekuja kwa mganga na walikuwa na magari yao.

Na bango la mganga walilitoa na kila kitu chake wakaondoa kila kitu wakachoma uwanjani. Na tukaomba nae na alipokuwa kwenye madhababu wenzake walishindwa kuingia ndani.

Na hii iwasaidie wahudumu na wachawi wenzie walipokuja kumsaidia walikuwa hawaoni mtu na walikuwa wanaona miali ya moto. *Na kwa habari za malaika asema, Afanyaye malaika zake kuwa pepo, Na watumishi wake kuwa miali ya moto. Waebrania 1:7*

Na hata mapepo yanakuwa hayaoni watu yataona moto tu. Hata wachawi walipokuwa wanatafuta kuingia walishindwa. Kwa hiyo biblia inaposema kuwa hili ni lango ina maana ni eneo maalumu la kuingilia.

Kwa hiyo hadi sasa huyu ni mtumishi wa Mungu na mchungaji sasa. Sasa turudi kwa Yakobo, chukulia huyu Yakobo angekutana na miungu mingine ingekuaje?

Sasa twende kwa mtoto Samuel na nafuatilia kwenye maandiko na sijaelewa bado kwanini aliwekwa karibu na sanduku la agano. Maandiko yanasema alipompeleka hekaluni na Kuhani Eli alimpeleka karibu na Sanduku la agano sasa kama unalala karibu na sanduku la agano utalala kweli? Biblia inasema kuwa akaanza kusikia sauti, maana kuna watu huwa usiku wakilala wanasikia sauti. Sasa ile sauti ilikuwa ni ya Mungu.

Sasa fikiria unaenda kulala hotel na unalala sehemu mtu kasahau hirizi yake hapo na wewe unakuja speed kuwa na hujaombea hapo. Sasa lazima utaota ndoto ngumu ngumu ivi.

SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA UWANJA WA BARAFU.

Na Babeli, huo utukufu wa falme, uzuri wa kiburi cha Wakaldayo, utakuwa kama Sodoma na Gomora hapo Mungu alipoiangamiza. Hautakaliwa na watu tena kabisa, wala watu hawatakaa ndani yake tangu kizazi hata kizazi. Mwarabu hatapiga hema yake huko, wala wachungaji hawatalaza makundi yao huko. Lakini huko watalala hayawani wakali wa nyikani; na nyumba zao zitajaa bundi; mbuni watakaa huko; na majini watacheza huko. Na mbwa-mwitu watalia ndani ya ngome zake; na mbweha ndani ya majumba ya anasa; na wakati wake u karibu kufika, na siku zake hazitaongezeka. ISAYA. 13:19-22 SUV

📖 Hii ni adhabu iliyotolewa katika mji wa Babeli na Mungu Mungu aliweka zuio na aliweka na wanyama wakali na majini yacheze ndani yake na mbwa mwitu walie huko ndani.

📖 hujawaji jiuliza kwanini mtu anaota ndani kwake kuna nyoka au jogoo au myama yoyote? Na ukiamka ni unasema ni ndoto tu na Mungu anakuambia kuwa hapa kuna shida.

Kuna mtu aliota mbwa kalala kwenye kitanda chake. Na majini yapo pale kisheria na huwezi nyamazisha maana wapo pale kihalali na ukitaka kuwatoa pale lazima uwe na **eviction order** ya mahakama ya mbinguni. Kwa hiyo lazima utumie neno la Mungu kisheria.

Na nilikuambia kuwa kila picha unayoota ina maana yake. Ukiona nyoka kuna maana yake ukiona mbuni kuna maana yake.

Kuna mtu alikuwa anaombea nyumba yake na kila akilala alikuwa anaona nyoka kweye ndoto na akiamka anawakuta kweli mara mlangoni na akiamka anakutana na nyoka kweli. Na aliuza zaidi ya nyoka 30 na wote wana rangi ya kufanana. Nenda kwenye biblia kuna mifano na mifano.

Kuna wakati wana wa Israel walitolewa Samaria.

Naye mfalme wa Ashuru akaleta watu kutoka Babeli, na Kutha, na Ava, na Hamathi, na Sefarvaimu, akawaweka katika miji ya Samaria badala ya wana wa Israeli; wakaumiliki Samaria, wakakaa katika miji yake. Basi ikawa, wakati ule walipoanza kukaa huko, hawakumcha BWANA; kwa hiyo BWANA akapeleka simba kati yao, nao wakawaua baadhi yao. Kwa hiyo wakamwambia mfalme wa Ashuru, wakasema, Wale wa mataifa uliowahamisha, na kuwaweka katika miji ya Samaria, hawajui kawaida ya Mungu wa nchi; kwa hiyo amepeleka simba kati yao, na tazama, wanawaua, kwa sababu hawajui kawaida ya Mungu wa nchi. Ndipo mfalme wa Ashuru akatoa amri, akasema, Mpelekeni mmojawapo wa makuhani, mliowachukua kutoka huko; aende akakae huko, akawafundisha kawaida ya Mungu wa nchi. Basi mmoja wa makuhani waliochukuliwa kutoka Samaria akaenda akakaa katika Betheli, akawafundisha jinsi ilivyowapasa kumcha BWANA. Lakini pamoja na hayo watu wa kila taifa wakajifanyia miungu yao wenyewe, wakaiweka katika nyumba za mahali pa juu, walipopafanya Wasamaria, kila taifa katika miji yao walimokaa. 2 WAFALME. 17:24-29

Baada ya kuraruliwa na simba walisema kwa sababu hatujui kawaida ya Mungu wa eneo hili. Ndio maana kuna wengine wanaota wanakimbizwa na nyoka au mbwa au wanyama wakali hivi.

Cha kufanya ni ombea kwanza mahali pako pa kulala na Mungu anakuambia kuwa mungu wa eneo hili ana alama hii. Na kama wewe ni mpangaji na hujafuatilia uwe na uhakika kuwa utaondolewa hilo eneo kama ni kwako patakukinai na uwe na uhakika kuwa utahama.

MAMBO YA KUFANYA KAMA UMEKUTANA NA HALI YA NAMNA HIYO.

1.Omba toba kama kuna kitu kiko mahali hapo na hakimpendezi Mungu. Omba toba . Na nilikufundisha namna ya kuzia ndoto mbaya kuwa ombea

👉 Nyumba unayolala

👉 Ombea mbingu

👉 Au mtu huyo anayeingia kwako. Jana nilikuambia habari za yule mama alivyoenda watembelea watoto wake na kwenda na mambo ya giza.

👉 Secure chumba cha kwako. Ombea hicho tu.

👉 Ombea ardhi ya hapo.

👉 Zuia kwa damu ya Yesu ndoto mbaya

Kama uko hotel ombea mahali pako tu usianzishe ugomvi bila sababu.

Siku moja tulikuwa Caltonia kwenye mkutano wa uchumi. Na sisi tuliwahi siku nne kabla. Sasa tulifika eneo la hollywood nadhani mnajua. Sasa unaweza kuelewa Mhubiri anaingia holly wood.

Na kama hujawahi muona shetani akitembea nenda pale. Na tukamuuliza Mungu tunafanyeje hapa.
Mungu alituambia jifunike kwa damu yangu.

Si unajua hata Yesu alikwepa vita, na sisi tulijiomba wenyewe. Sasa kama hujui namna ya kufanya mazingira ya namna hiyo unaweza kwama.

Mahali popote pale watu hawakai au nyumba au chumba ina maana kuna ukiwa na ukiwa ni adhabu. Unasafiri muda mrefu hata kama ni kwako jifunze kuomba maana unaweza kutana na vitu vigumu.

2. Mwaga damu ya Yesu kwenye eneo unalokaa au unalolala

Damu ikimwagika huwa inaondoa kila kilichoko hapo.fanya zoez nyumbani kwako. Na kuna kijana mmoja alisikia hili somo na yeye akaenda akamwaga damu ya Yesu nyumbani kwake na aliweza kuomba maana mara ya kwanza alikuwa hawezi.

Mwingine alikuwa anashindwa kulala lakini baada ya kumwaga damu ya Yesu eneo lake aliwaza kulala vizuri.

3.Hakikisha unakemea nguvu za giza zilizoko mahali pale

Kama watu wamelala hapo na wamefanya uasherati na eneo hilo hilo, juzi nilikuambia sabuni haiondoi nguvu za giza. Na unashangaa unalala hapo na mapepo yanaanza kukusumbua.

Kwa hiyo ombea na mashuka kwa damu ya Yesu maana damu ya Yesu husafisha kabisa.

4 Ombea uwepo wa Roho Mtakatifu na malaika zake

Neno la Mungu linasema **Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa.Zaburi 34:7**

Kwa hiyo malaika wanaweza kukufanyia ulinzi.

SEHEMU YA PILI

ENEO ULILOWAHI KULALA NA UKAONDOKA KATIKA HIMAYA YA MAPEPO

*Biblia inasema Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni **juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.** Waefeso 6:12*

☞ Hiyo ni ngazi yao sasa jeshi la pepo wabaya wana vikosi vyao. Na nilishangaa siku moja niliona makundi Tofauti Tofauti ya malaika. Na wanakuwa miili Tofauti wale wa kuligana na kazi iliyopo. Wale wapiganaji hawana mabawa ila wanakuwa na Farasi weupe. Na wengine wana maumbo ya kwao. Na wale wanaoimba nao wana sura tofauti. Ni mara chache huwa nawaona, na muda mwingine na wao wanakuja kuimba na sisi.

Ukisoma Mwanzo 28:10-17 ☞ angalia 28 ☞

*Yakobo akaondoka asubuhi na mapema, akalitwaa lile jiwe aliloliweka chini ya kichwa chake, akalitimamisha kama nguzo, na kumimina mafuta juu yake. **Akaita jina la mahali pale Betheli;** lakini jina la mji ule hapo kwanza uliitwa Luzu. Yakobo akaweka nadhiri akisema, Mungu akiwa pamoja nami, akinilinda katika njia niiendeayo, na kunipa chakula nile, na nguo nivae; nami nikirudi kwa amani nyumbani kwa baba yangu, ndipo BWANA atakuwa Mungu wangu. Na jiwe hili nililolisimamisha kama nguzo litakuwa nyumba ya Mungu; na katika kila utakalonipa hakika nitakutolea wewe sehemu ya kumi. MWANZ. 28:18-22 SUV*

***Na malaika wa Mungu akaniambia katika ndoto, Yakobo! Nikasema, Mimi hapa.** Akasema, Inua, basi, macho yako, ukaone; mabeberu wote wanaopanda wanyama wana milia, na madoadoa, na marakaraka; maana nimeona yote aliyokutendea Labani. **Mimi ni Mungu wa Betheli,** huko ulikotia mafuta nguzo, na kuniwekea nadhiri. Sasa ondoka, toka katika nchi hii, urudi mpaka nchi ile uliyozaliwa. MWANZO. 31:11-13 SUV*

*Mungu akamwambia Yakobo, **Ondoka, panda uende Betheli, ukakae huko; ukamfanyie Mungu madhabahu huko;** yeye aliyekutokea ulipomkimbia Esau, ndugu yako. Yakobo akawaambia watu wa nyumbani mwake, na wote waliokuwa pamoja naye, Ondoeni miungu migeni iliyoko kwenu, mjisafishe mkabadili nguo zenu. Tuondoke, tupande kwenda Betheli, nami nitamfanyia Mungu madhabahu huko; yeye aliyenisikia siku ya shida yangu, akawa pamoja nami katika njia yote niliyoiendea. MWANZO. 35:1-3 SUV*

Sasa kwanini Mungu alitaka kumkubusha **kuwa Mungu wa Betheli.** Na kila mahali nilienda na wewe na malaika wangu. Sasa fikiria Yakobo angekutana na mapepo?

Mungu anataka kuingia kwenye agano. Mara nyingi huwa nawaambia watu kuwa kama unaota ndoto unakula na watu waliokufa kwenye ndoto usiowajua au unakula nyama ambayo sio kawaida kula. Maana yake ni kuwa unaingizwa kwenye agano na mapepo yako pale

Kama Malaika alimfuata Yakobo kwa Labani na alimkumbusha kurudi Betheli. Na kama ulikutana na mapepo yaani ulilala shule na hapakuwa pazuri kuna mapepo yataanza kukufuatilia. Kuna mapepo yanaitwa Demon monitors na kila mahali yanakufuatilia. Miaka na miaka na unaota ndoto uko shule. Sasa kumbuka kukata kitu cha kiroho ulicho kutana nacho mahali hapo maana itakutesa.

**SEMINA YA NENO LA MUNGU DODOMA NA MWL MWAKASEGE TAR 2-9 APRIL 2017. DODOMA
UWANJA WA BARAFU.**

Jifunze namna ya kujikung'uta maana unaweza ukaokota kitu hotelini na inanza kuhamia kwako. Cheki unamtembelea mwenzio na unakuta ugomvi wa nyumbani kwa rafiki yako na unahamia kwako na unanza kufanana fanana na kule.

Kwa hiyo hakikisha unakata hiyo connection kwa damu ya Yesu. Jikung'ute kila mahali ulipotoka hata kama mtu amekuja kukutembelea kwa kwako hakikisha unaomba na kung'uta kila kitu anachokuja nacho.

Hujawahi ona umeota ndoto katika mazingira mbali mbali na uko sehemu tofauti tofauti. Mara uko Morogoro na Dar es Salaam au Dodoma. Hiyo ni Mungu anataka kukumbia kuwa kata hiyo connection.

Ninaona mtu aliachiwa alama mkononi kwenye ndoto na nyoka ulipolala. Na kuna pepo lipo linakufatilia na kila ukienda mahali popote una tembea nalo. (Mwl alifanya maombi ya mtu huyo na kukata hiyo network.) Na pepo lilipuka na kumtoka huyo mtu.

Hili lilikuwa ni zoezi ili kuthibitisha kitu alichokuwa anafundisha. Kwa hiyo jifunze namna ya kuomba toba. Na sasa nakata connection ya hilo pepo na baada ya maombi mtu alifunguliwa.

Tunakwenda sawa sawa.?

WEKA MKONO WAKO JUU YA MAGOTI NA MAHALI ULIPOLALA NA ARDHI INAKUMBUKA.

NA NAOMBEA ENEO LOLOTE AMBALO UNALALA NA UKIWAHI KULALA NA NAACHILIA DAMU YA YESU.

KAMA KUNA KITU NYUMBANI KWAKO CHA KAMBI NYINGINE KAKITOE MAANA NAMWAGA DAMU YA YESU SASA HIVI KWA KILA ANAYEFUATILIA SOMO HILI

MAOMBI NA BARAKA.

Pia kama hujampokea Yesu hakikisha unaokoka na kumpata Yesu. Soma kitabu pale juu cha hongera kwa kuokoka.

Pia tembelea www.mwakasege.org na angalia eneo la chini utaona alama ya Facebook like pale na utakuwa unapa masomo kwa njia ya Facebook.

Pia somo hili la ndoto linaendelea Facebook kwenye ukurasa wa Christopher & Diana Mwakasege (Mana Ministry)

Ubarikiwe sana sana na tuonane tena semina ijayo

Noted by

***Felix Hezrone Mbwani +255716918848 & Glory Mlay +255655751681**

felixmbwani@gmail.com